

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 1 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

*(Hapa Kwaya ya Bunge iliimba Wimbo wa Taifa na Wimbo
wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)*

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge ninaomba utulivu tunalo
jambo zito mbele yetu.

Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA KUJIUZULU KWA SPIKA

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 6 Januari, 2022 nilipokea
taarifa ya kujiuzulu kwa Spika wa Bunge Mheshimiwa Job
Yustino Ndugai na ninaomba niiwasilishe kwenu kama
ifuatavyo:-

Imeandikwa tarehe 6 Januari, 2022 imeelekezwa kwa Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, Katibu wa Bunge Sanduku la Posta 941, Dodoma. Kichwa cha Habari ni kujuzulu nafasi ya Uspika.

Naomba kukujulisha kuwa nimeamua kujuzulu nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 6 Januari, 2022. Uamuzi huu ni wa hiari na umezingatia maslahi mapana ya Taifa, hivyo kwa kuzingatia masharti ya Ibara 149(1)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, nawasilisha uamuzi wangu huo ili...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninaomba utulivu tuna jambo zito sana mbele yetu.

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Hivyo, kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 149(1)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, nawasilisha uamuzi wangu huo ili ultaarifu Bunge katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano ujao wa Bunge kwa hatua stahili za kujaza nafasi hiyo. Nawasilisha. Imesainiwa na Job Yustino Ndugai, Mbunge na nakala imetumwa kwa Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Taifa - Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 149(1)(c) iliyotajwa kwenye taarifa ya Mheshimiwa Job Ndugai pamoja na mambo mengine inaelekeza kwamba mtu ye yeyote mwenye dhamana ya kazi yoyote iliyoanzishwa na Katiba anaweza kujuzulu kwa kutoa taarifa iliyoandikwa na kutiwa sahihi kwa mkono wake kwa kufuata masharti kwamba iwapo mtu huyo ni Spika basi taarifa hiyo ya kujuzulu ataiwasilisha kwenye Bunge.

Aidha, Ibara ya 149(2) pamoja na mambo mengine inafafanua kwamba mtu aliyetoa taarifa ya kujuzulu kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 149(1) atahesabiwa kuwa

amejiuzulu tangu siku ile ambayo taarifa yake ya kujiuzulu itakapopokelewa na mtu ye yote aliyeruhusiwa kupo kea taarifa hiyo na mtu anayehusika au kikao kinachohusika.

Kiutaratibu, taarifa na nyaraka zinazowasilishwa Bungeni hupo kelewa na Katibu wa Bunge. Hivyo kwa taarifa hiyo ya Mheshimiwa Ndugai na kwa mujibu wa Ibara ya 149(2), Kiti cha Spika kimekuwa wazi kuanzia tarehe 6 Januari, 2022 taarifa hii ilivyopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine jana tarehe 31 Januari, 2022 saa 12.00 jioni nilipokea taarifa ya kujiuzulu kwa Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na taarifa hiyo naomba niiwasilishe kwenu kama ifuatavyo:-

Imeandikwa tarehe 31 Januari, 2022 imeelekezwa kwa Nenelwa J. Mwihambi, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sanduku la Posta 941, Dodoma. Inahusu taarifa ya kujiuzulu nafasi ya Naibu Spika; tafadhalii husika na kichwa cha habari hapo juu, napenda kukufahamisha kwamba kufuatia nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa wazi, chama changu cha siasa - Chama cha Mapinduzi (CCM), kimeniteua kugombea nafasi ya Spika katika uchaguzi utakaofanyika tarehe 1 Februari, 2022. Kwa hali hiyo, ninajiuzulu nafasi ya Naibu Spika wa Bunge kuanzia tarehe 31 Januari, 2022. (*Makofi*)

Hivyo, nawasilisha kwako taarifa hii ya kujiuzulu ili kukidhi masharti ya Ibara ya 149(1)(c) na Ibara ya 149(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imesainiwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Naibu Spika na nakala inakwenda kwa Daniel Godfrey Chongolo, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tarehe ya uchaguzi na taratibu zote kuhusiana na uchaguzi wa Naibu Spika tutaleta kwenu baadaye Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu wa shughuli inayofuata.

NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI:

UCHAGUZI WA SPIKA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 84(8) ya Katiba inaelekeza kwamba Kiti cha Spika kitakapokuwa wazi hakuna shughuli yoyote itakayotekelawa katika Bunge isipokuwa uchaguzi wa Spika. Hivyo ili shughuli za Bunge ziendelee katika Mkutano huu inatakiwa tuanze na uchaguzi wa Spika. Sasa ninamuita Katibu ili atupe maelezo ya utaratibu wa uchaguzi wa Spika. Katibu!

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mchakato wa uchaguzi wa Spika umewekewa utaratibu kwenye Kanuni ya 9 na Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni za Bunge Toleo la Juni, 2020. Pamoja na mambo mengine Kanuni ya 9 inaelekeza kwamba uchaguzi wa Spika utafanyika katika mazingira yafuatayo:-

Kwanza; ni Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge jipya mara baada ya Katibu kusoma Tangazo la Rais na kikao hicho kujigeuza kuwa Mkutano wa Uchaguzi wa Spika, au kikao kinachofuata cha Mkutano wowote wa Bunge mara baada ya Kiti cha Spika kuwa wazi ambacho ndiyo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 9(5) inaelekeza kwamba uchaguzi wa Uspika utasimamiwa na Mwenyekiti ambaye atatoka miongoni mwa Wabunge ambao wamekuwa Wabunge mfululizo kwa muda mrefu na asiye mgombea wa nafasi ya Spika baada ya kuombwa na Katibu kuongoza Mkutano wa Uchaguzi wa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumbukumbu za ofisi kwa sasa Mbunge ambaye amekuwa Mbunge mfululizo kwa

muda mrefu na ambae siye mgombea wa nafasi ya Uspika ni Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi. Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi amekuwa Mbunge mfululizo kuanzia mwaka 1995, hivyo kwa muda muafaka nitaomba kikao hiki kijigeuze kuwa Mkutano wa Uchaguzi wa Spika na kufanya uchaguzi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii sasa tumekamilisha shughuli za awali za Kikao cha Bunge, hatua inayofuata ni Mkutano wa Uchaguzi wa Spika ambao utaongozwa na Mwenyekiti wa Uchaguzi kama ilivyoelekezwa na Katibu wa Bunge. Kwa sababu hiyo sasa ninaahirisha Kikao cha Bunge ili kutoa nafasi kwa Mkutano wa Uchaguzi wa Spika kufanyika, baada ya hapo Spika atakayechaguliwa ataingia Bungeni kwa utaratibu wa kawaida ili kuongoza shughuli za Bunge zinazofuata. (*Makofi*)

(Hapa Bunge lilisitishwa kupisha shughuli za Uchaguzi wa Spika)

MKUTANO WA UCHAGUZI WA SPIKA

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE: Waheshimiwa Wabunge, wakati mmesimama naomba kwa heshima na taadhima nimuombe Mheshimiwa William Lukuvi ajongee hapa mbele kwa ajili ya kutuongozea Mkutano wetu. (*Makofi*)

Hapa (Mhe. William V. Lukuvi) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mnajua mkishangilia sana naweza nikagoma kutoka hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa

Wabunge na waalikwa waliomo humu ndani ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WABUNGE FULANI: Kazi iendelee.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyo sika maelezo ya awali kazi iliyo tuleta leo ni Uchaguzi wa Spika, lakini kabla hatujaingia kwenye jukumu hilo naomba nirudie maneno ambayo ameyasema Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai sisi sote na kutuvusha kutoka mwaka 2021 kuingia mwaka 2022 maana hatujaonana, pia nimuombe Mwenyezi Mungu atupe hekima ili hili jambo tunalotarajia kulifanya tulifanye kwa busara na hekima. (*Makofii*)

Lakini niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa mlivo fanya mwishoni mwa mwaka huu. Najua Wabunge wengi hapa wametoka majimboni na kazi kubwa huko majimboni tulikuwa tunafanya ni kusimamia kazi na pesa zilizopelekwa huko, hasa katika kazi ya ujenzi wa madarasa 15,000 ambayo ni historia na rekodi. (*Makofii*)

Tumekuwa tunajenga katika awamu zote sekondari, lakini ubunifu wa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mama Samia Suluhu Hassan umetuwezesha kujenga madarasa ambayo yamemaliza mahitaji ya sasa ya wanafunzi wetu kwenda kidato cha kwanza, madarasa 15,000 kwa mpigo na mimi najua baadhi yetu tumeshiriki vizuri sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kazi hii imefanywa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya wananchi, lakini najua na sisi Wabunge kazi hii imetubebea sana kwa sababu hakuna kazi kubwa ya heshima ambayo imefanyika kubwa kwa wakati mmoja kama hii.

Kwa hiyo, tunayo kila sababu Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza jambo hili tujipongeze, lakini tumpongeze na Mheshimiwa Rais kwa kutubeba. Basi, simameni kabisa mumpongeze. (*Makofii*)

(Hapa Wabunge walismama na kupiga makofi kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

WABUNGE FULANI: CCM, CCM.

MWENYEKITI: Ahsanteni sana, kama mnavyojua haya mambo ambayo tumeyafanya na Mheshimiwa Rais ameyafanya yamefanywa bila ubaguzi. Madarasa haya yamejengwa Nkasi, yamejengwa Dar es Salaam, yamejengwa kila mahali. Kazi hizi kubwa za kimapinduzi zimefanywa bila ubaguzi wa kijinsia, dini, eneo, wala siasa, kwa hiyo, tunao kila wajibu wa kumpongeza Mheshimiwa Rais. Sisi ni wawakilishi wa wananchi na ndoto zenu bila ya shaka na ninyi mngependa mdumu kama alivyodumu Mwenyekiti anayeongoza kikao cha leo. Sasa njia ni hii, mama amewafagilia mshindwe wenyewe. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi niombe sana ushirikiano, tunayo kazi kubwa ya kufanya leo na ya heshima. Maelezo ya utangulizi yamesema tunakuja kuchagua Spika, kiongozi wa mhimili wetu, kwa hiyo, nadhani kila mmoja atatumia busara, atatumia haki yake ya kikatiba kufanya uchaguzi ulio bora.

Kwa hiyo, baada ya maelezo haya naomba nimuite sasa Katibu wa Bunge ambaye ndio msimamizi na mwelekezi wa uchaguzi huu aweze kutoa maelezo yanayofuata. Karibu Katibu wa Bunge. (*Makofi*)

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Ibara ya 84 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Spika wa Bunge anachaguliwa na Wabunge kutoka mionganini mwa Wabunge au watu wenye sifa za kuwa Wabunge. Aidha, Katiba inaelekeza kwamba uchaguzi wa Spika utafanyika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza

wa Bunge jipya au katika Kikao cha Kwanza chochote mara baada ya kutokea Kiti cha Spika kuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoarifiwa hapo awali, Kiti cha Spika wa Bunge hili kimekuwa wazi kuanzia tarehe 6 Januari, 2022. Tarehe 7 Januari tulitoa taarifa kwa vyama vyaya siasa vyenye usajili wa kudumu vinavyokusudia kusimamisha mgombea katika uchaguzi wa Spika vianze mchakato wa ndani wa kuwapata wagombea wao. Aidha, tarehe 8 Januari, 2022 tulitoa Tangazo Namba 12B katika Gazeti la Serikali kuujulisha umma kuwa uchaguzi wa Spika utafanyika tarehe 1 Februari, 2022 ambayo ni siku ya kwanza ya Mkutano wa Bunge baada ya nafasi ya Spika kuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa hizo tulifafanua kuwa chama kinachokusudia kusimamisha mgombea ambaye sio Mbunge kiwasilishe jina la mgombea huyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi siku tano kabla ya uchaguzi ili Tume ifanye uchambuzi na kujiridhisha iwapo mgombea huyo ana sifa za kuwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba na Tume itawasilisha majina kwa Katibu wa Bunge siku mbili kabla ya uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, hadi kufikia saa 10.00 jioni siku ya Jumatatu, tarehe 31 Januari, 2022 ambayo ilikuwa ndio siku ya uteuzi nilikuwa nimepokea majina ya wagombea tisa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kwanza ni Bwana Abdullah Mohamed Said kutoka Chama cha NRA, wa pili ni Engineer Aivan Jackson Maganza kutoka Chama cha TLP, wa tatu ni Bwana David Daud Mwaijojele kutoka Chama cha CCK, wa nne ni Bwana Georges Gabriel Bussungu kutoka Chama cha ADA-TADEA, wa tano ni Bwana Kunje Ngombale Mwiru kutoka Chama cha SAU, wa sita ni Bi. Maimuna Said Kassim kutoka Chama cha ADC, wa saba ni Bwana Ndonge Saidi Ndonge kutoka Chama cha AASP, wa nane ni Bwana Saidoun Abrahamani Khatibu kutoka Chama cha DP na wa tisa ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kutoka... (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie; wa tisa ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kutoka Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwataarifu kuwa wagombea hawa wote wamekidhi masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Sasa naomba kuainisha kwa kifupi utaratibu utakaotumika kwenye zoezi la Uchaguzi wa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu uliowekwa na Bunge hili kila mgombea atatakiwa kufika mbele ya Wabunge ili kujieleza, kuulizwa maswali na kujibu maswali kama yatakuwepo pamoja na kuomba kura. Baada ya zoezi hilo kukamilika kila Mbunge atapewa karatasi ya kura yenye majina ya wagombea husika na atatakiwa kumpigia kura ya siri mgombea mmoja tu kwa kuweka alama ya vema pemberi ya jina lake na kutumbukiza katika sanduku la kupigia kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 9(9)(i) cha Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni mgombea atakuwa amechaguliwa kuwa Spika iwapo atapata zaidi ya nusu ya kura za Wabunge wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapiga kura katika uchaguzi huu ni Wabunge wote. Aidha, Ibara ya 68 ya Katiba inaruhusu Mbunge ambaye hajaapishwa kushiriki kwenye zoezi la uchaguzi wa Spika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo mionganoni mwetu leo tuna Mbunge mpya wa Jimbo la Ngorongoro ambaye bado hajaapishwa, lakini kwa kufuata masharti ya ibara hiyo ya Katiba ni mpiga kura halali kwenye uchaguzi wa Spika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya naomba sasa nikukaribishe ili tuanze rasmi shughuli ya

uchaguzi, hata hivyo kwa kuwa wagombea nane wa nafasi ya Spika sio Wabunge naomba uridhie Kanuni zitenguliwe ili muda utakapofika waruhusiwe kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kushiriki zoezi la kujieleza na kupigwa kura.

Mheshimiwa Mwneyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Katibu wa Bunge na kwa kuwa kutakuwa na wagombea ambao si Wabunge, nitamuita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera, Bunge na Uratibu ili aweze kutengua Kanuni za Bunge ili kuruhusu wagombea hao kuingia kwa sababu kwa utamaduni wa kugombea itabidi waingie humu ndani wajieleze. Sasa ili wapate fursa hiyo nakukaribisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, ili iwawezeshe hao wagombea wengine waweze kuingia ndani kujieleza na kuomba kura.

Kabla hujasema naomba niwahoji Wabunge ambao wanaafiki hoja hii waseme ndio.

(Hoja ilitolewa na Kuamuliwa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri karibu. Toa hoja kwanza halafu nitawahoji tena. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, BUNGE

NA URATIBU: Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa kuwa, Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 inaweka masharti kwamba Spika atachaguliwa na Wabunge kutoka mionganoni mwa watu amba ni Wabunge au mtu mwenye sifa za kuwa Mbunge.

Na kwa kuwa, kikao hiki kinakusudia kumchagua Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 9(1) ya Kanuni za Bunge za Kudumu, Toleo la Juni, 2020.

Na kwa kuwa, Bunge hili limejiwekea uratatuwa wa kuwaruhusu wagombea wa nafasi ya Spika kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kujitambulisha kwa wapiga kura, yaani Wabunge, kujieleza na kuomba kura.

Na kwa kuwa, Kanuni ya 160 ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaweka utaratatuwa maalum kwa Wabunge, watumishi na wageni kukaa kwenye ukumbi wa Bunge.

Hivyo, basi kwa mujibu wa Kanuni ya 174(1) naomba kutoa Hoja ya Kutenga Kanuni ya 160 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kuwaruhusu wagombea wa nafasi ya Spika ambaao sio Wabunge kuingia kwenye ukumbi wa Bunge kushikiri uchaguzi wa Spika wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagombea hao ni kama ifuatavyo; wa kwanza ni Bwana Abdullah Mohamed Said – NRA; wa pili ni *Engineer Aivan Jackson Maganza* kutoka Chama cha TLP; wa tatu ni Bwana David Daud Mwaijolele kutoka Chama cha CCK; wa nne ni Georges Gabriel Bussungu – ADA-TADEA; wa tano ni Bwana Kunje Ngombale Mwiru kutoka Chama cha SAU; wa sita ni Bi. Maimuna Said Kassim kutoka Chama cha ADC; wa saba ni Bwana Ndonge Saidi Ndonge kutoka AAPF na wa nane ni Bwana Saidoun Abrahamani Khatibu kutoka DP.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Naomba niwahoji, wale ambaao wanaafiki hoja iliyotolewa na Balozi Dkt. Pindi Chana waseme ndiyo. Wale ambaao wote mmesema ndio eeh? Haya na wale ambaao wanafikiri uchaguzi uahirishwe labda. Wanaosema siyo? (*Kicheko*)

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

MWENYEKITI: Baada ya maelezo haya, sasa tunaingia kwenye kazi, kazi hizi tulimo humu ndani tumezoea sana maana tumezoea kuchaguliwa. Kwa hiyo, ningeomba

tukubaliane mambo machache ya msingi; hawa watu ni wengi, lakini kila mtu lazima apate fursa sawa, lakini kanuni imeshatenguliwa wataingia hapa ndani, tukubaliane maelezo ya kila mmoja yachukue dakika ngapi?

Kwa kawaida humu ndani huwa tunachukua dakika tatu. Sijui kama mnaafiki waendelee kujieleza kwa dakika tatu?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, watajieleza kwa dakika tatu kila mmoja, lakini pili kuna utamaduni wa kuuliza maswali, mnapendekeza maswali yaulizwe mangapi kwa kila mmoja? Moja? Mawili? Matatu?

WABUNGE FULANI: Ndiyo!

MWENYEKITI: Kwa hiyo, kila mmoja ataulizwa maswali matatu, kama yapo. Humu ndani Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson yupo kwa sababu yeye ni Mbunge amekaa humu ndani, lakini wale wengine tumewawekea mahali watasubiri, wataitwa mmoja baada ya mwingine. Kwa hiyo, baada ya hapo sasa tunaanza kazi.

Wale ambao hawajawahi kufanya kazi ya uchaguzi ndio wanasema maneno hayo. Yeye ni mpiga kura, ni Mbunge, hawezи kutoka humu ndani. (*Makofii*)

Haya, baada ya hapo naomba nianze sasa kuwaita mmoja-mmoja. Aje Bwana Abdullah Mohamed Said wa NRA.

(Hapa Bwana Abdullah Mohamed Said Aliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Bwana Abdullah Mohamed Said kutoka Chama cha NRA umeteuliwa na Tume ya Uchaguzi kuja kugombea nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hawa ndio wapiga kura. Kwa hiyo, utapata fursa ya kujieleza kwa dakika tatu na kuomba

kura, lakini tumekubaliana humu ndani utaweza kuulizwa maswali matatu kama yapo.

Hata hivyo, kabla hujaanza, Mgombea wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Tulia nikucombe tu ili na wengine waridhike kwamba wanapojieleza hawa wote, ukae nje, lakini baada ya maelezo, utarudi ndani utakapoitwa zamu yako utaingia. (*Makofi*)

Hapa (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alitoka Ukumbini

MWENYEKITI: Haya Wajumbe, tusikilize kidogo, maana hata sisi huwa tunachaguana hivi hivi na ninyi leo mmekuwa Wajumbe na Wagombea ndio hawa hapa.

Haya Mheshimiwa Bwana Abdullah Mohamed Said, karibu.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote kwanza niwasalimieni kwa salamu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WABUNGE FULANI: Kazi iendelee.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: *Asalaam Aleykum Warahmatullah Wabarakatuh.*

WABUNGE FULANI: *Waaleykum Salaam.*

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Bwana Yesu Asifiwe.

WABUNGE FULANI: Amen.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah-Wataala*, muumba na muweza wa kila jambo, hakika yeye ndiye mfanyaji wa kila kitu na nafsi zetu ziko kwenye mkono wake, kwa kunijaalia leo kuzungumza mbele

yenu Waheshimiwa Wabunge. Huu ni uwezo wa Mwenyezi Mungu wala siyo uwezo wa yeoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nawashukuru viongozi wangu walioniwezesha pia leo kuwepo hapa. Vilevile napenda kumshukuru sana mke wangu...

MBUNGE FULANI: Ehe!

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAIDI: ...mwandani wangu Bi. Beatrice Thomas Mchome... (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Jamani, utulivu eeh!

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAIDI: ...kwa jina lingine ni Rahma Thomas Mchome, kwa kunipa ujasiri na kunipa moyo na kunihakikishia kwamba kwa kadri ninavyokufahamu kwa ufanisi na uwezo ulionao unakuja kuwa Spika, unawashinda wote. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri na Waheshimiwa wageni waalikwa, kwa jina naitwa Abdallah Mohamed Saidi, mzaliwa wa katika Jimbo la Uchaguzi la Ziwanii, Chakechake Pemba. Katika uchaguzi wa mwaka 2020 nilikuwa pia mgombea wa Ubunge katika Jimbo hilo na nilipata kura nyingi. (*Makofi*)

Waheshimiwa dakika hazitoshi, kama ningeulizwa ningesema nahitaji dakika angalau 20, lakini sisi tunataka heshima katika Bunge letu liwe ni Bunge bora Afrika. Hili litawezekana mkinichagua mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu langu nikiwa ni Spika nitawaongoza Wabunge kwa ufanisi na kuwaweza kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Namna ya kuwaongoza na kutekeleza na kuwaweza nitaweza. Mkiniuliza swali hili nitakuja kufanua. Tunahitaji kumuunga mkono na kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ni tabia siyo nzuri kama wasimamizi wa maendeleo na Serikali, sisi wenyewe kwanza tukaanza kugombana, jinsi gani tunaijenga nchi yetu? Hii ni nchi yetu, ni lazima tusimame kutetea nchi yetu katika hali yoyote. Tusimpe nafasi yejote ya kutuhujumu katika nchi yetu. Kwa hiyo, kila jambo ni lazima ninyi Wabunge na watendaji tuwe karibu na Rais kwa ajili ya kumsaidia na siyo kumkwaza au kumkatisha tamaa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, dakika ni chache, lakini naamini nimekuja hapa siyo kushiriki, nimekuja kushinda. (*Makof*)

Nina hakika kabisa kwamba chama changu hakina Mbunge hapa, lakini ninaamini watu waliomo humu ni waelewa na ni watu wenye saikolojia ya hali ya juu kabisa. Kwa hiyo, ninaamini kwa kusimama hapa tu na maneno ninayozungumza watapenda kupata maendeleo na Bunge letu liwe bora Afrika. Kwa hiyo, hawatasita kunipa kura zao, naomba kura zenu. Naomba nipate kura 393 bila kupungua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana.

Ndugu Abdullah Mohamed Said amemaliza kujieleza, kama kuna Mheshimiwa yejote anataka kuuliza swali.

MHE. AGNES M. MARWA: Agnes.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Agnes nimekuona.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa umahiri wako wa kuendesha kikao hiki. Pia nampongeza sana Mheshimiwa mgombea kwa kweli yuko vizuri, anajitosheleza na anajiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeleo ya Mheshimiwa mgombea nimemsikia akisema kwamba nguvu

au power ya kuliongoza Bunge hili amepewa na mke wake na siyo chama chake. Sasa ningependa kumuuliza swalii. (*Kicheko*)

Naomba nirudie kidogo Mheshimiwa mgombea.

MWENYEKITI: Umeeleweka.

MHE. AGNES M. MARWA: Ametuelezea kwamba uwezo anaujua mke wako na nguvu anazijua mke wako na ndiyo maana akakupa nguvu ya kuja kugombea hii nafasi ya Uspika.

Sasa swalii langu; je, na sisi kama Wabunge, maana humu tuko Wabunge wanawake na wanaume usisahau; sasa hatujui kwanza ni nguvu gani hizo? (*Kicheko*)

Pili, utatuwezeshaje au uvezeshaji huo ni wa aina gani? Ni huo huo ambao mke wako anaujua? Ahsante. (*Kicheko*)

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ingawa siyo swalii kamili, lakini ukipenda unaweza kujibu.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Ahsante sana dada yangu Mheshimiwa Agnes kwa swalii lako hilo. Najua nimesema kwamba mke wangu ndio ameniwezesha; kule kwenye chama tulipambana, lakini viongozi na wengine wakaona kwamba mimi naweza kuja kuchukua kitii hicho cha Uspika bila mashaka yoyote, lakini kule nyumbani, tunasema hata kwa Kiswahili kwamba, "mwanaume mwenye mafanikio nyuma yake kuna mwanamke." (*Makofi/Vigelego*)

Kwa hiyo, siyo siri, mke wangu Beatrice Thomas Mchome amekuwa ni mshirika wangu, amekuwa ni mwenzangu, amekuwa ni rafiki yangu, anajua kila kitu changu na vilevile amekuwa ni mtu mwenye kujiamini na

kuniaminisha na pia anafahamu majukumu niliyoyafanya. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba sikupata nafasi ya kujieleza, nilitengeneza kipeperushi ambacho nilitaka kila mmoja akipate, ninavyo, lakini *logistic* haikukaa vizuri. Mngepata kunielewa mionganoni mwa kazi nilizofanya za kitaifa, kijamii na hata kimataifa katika kusimamia. Yeye anafahamu kwa sababu niko naye kwa zaidi ya miaka 20. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali kwa mgombea.

Mheshimiwa mgombea, Bunge letu linaendeshwa kwa mujibu wa kanuni na desturi mbalimbali. Kwanza najua wagombea wote mtakuwa mmezisoma Kanuni za Bunge. Naomba unitajie kanuni tatu muhimu ambazo Wabunge wamekuwa wakizitumia mara kwa mara.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAIDI: Mheshimiwa naomba jina lako.

MWENYEKITI: Hebu rudia kidogo, rudia.

MHE. ESTER A. BULAYA: Bunge linaendeshwa kwa mujibu wa kanuni, mila na desturi na taratibu ya Mabunge mbalimbali. Sasa najua wewe unagombea Kiti cha Uspika na kwa sababu Bunge letu linaendeshwa kwa kanuni, naamini utakuwa umepitia Kanuni za Bunge. Naomba unitajie kanuni tatu ambazo ni maarufu kwenye jumba hili Wabunge huwa tunatumia mara kwa mara. Ahsante. (*Makofi*)

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Ahsante sana Mheshimiwa Bulaya kwa swali lako hilo ambalo ndani yake

hasa ni swali la utendaji na utekelezaji, jinsi gani unasimamia Kanuni za Bunge na pia unataka nikutajie. Vilevile nikukumbushe kwamba siyo kwamba Bunge linaongozwa kwa kanuni na taratibu tu, pia kuna Katiba ndiyo inayoanza. Kwa ujumla ni kwamba mambo haya yalikuwa ni ghafla na nilikuwa niko mikoani... (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Haya, tuskilizane, tuskilizane. Malizia maelezo.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Mheshimiwa Bulaya, dada yangu, nilikuwa nafanya kazi kule Newala kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa korosho. Kwa hiyo, hawa viongozi wangu wenyewe, mimi nilikuja nikaandika barua nikawapelekea na kwa kweli nimetoka huko, nimefika Dodoma jana tu hapa ... (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Semea kwenye *microphone*.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Kwa hiyo, Mheshimiwa nafikiria utaelewa kwamba suala la kusoma kanuni, hilo ni jambo la mara moja tu, linawezekana kwa muda mchache na ninakuhakikishia nina kichwa. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana. Nafikiri hakuna swali lingine. Kwa hiyo, Bwana Abdullah Mohamed Said, tunakuruhusu.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAIDI: Ahsanteni. (*Makofii*)

(*Hapa Ndg. Abdullah Mohamed Said Aliondoka Ukumbini*)

MWENYEKITI: Ahsante. Haya aje mgombea namba mbili, *Engineer Aivan Jackson Maganza*. Huyu anatoka Chama cha TLP. Karibu. (*Makofii*)

(*Hapa Eng. Aivan Jackson Maganza Aliingia Ukumbini*)

MWENYEKITI: Bwana *Engineer* Aivan Jackson Maganza, umeomba nafasi ya Uspika. Mbele yako ni Waheshimiwa Wabunge ambao ndio wapiga kura. Unapewa dakika tatu kujieleza na pia Waheshimiwa hawa wanaweza wakakuuliza maswali matatu kama yapo, karibu.

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninashukuru kwa utaratibu wako unavyoliendesha Bunge, naona inaturidhisha sisi wote.

Kwa majina naitwa *Engineer* Aivan Maganza, ni Mwenyekiti wa Vijana TLP-Taifa, lakini pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu TLP-Taifa.

Ndugu Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa wote na Mawaziri mliopo ndani ya Bunge letu, naomba kuwasalimu kwa salamu yetu ya kitaifa, kazi iendelee. (*Kicheko/Makofi*)

Ndugu Wajumbe, nashukuru sana, nadhani ni kauli ya mama yetu mpPENDWA Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Nilitaka mmalizie mjisema, "kazi iendelee," nikiwa namwangalia Waziri Mkuu anasemaje naye? Naona anataka kazi iendelee. (*Makofi/Kicheko*)

Ndugu Wajumbe, kwa uzoefu wangu tu wa uongozi, naomba niseme nilikuwa Rais wa Chuo Kikuu, lakini pia nilikuwa Msemaji wa Vyuo Vikuu Tanzania. Kwa mwaka 2015 nilishiriki katika kampeni ya kitaifa ya kumpigia kura Hayati Dkt. John Pombe Magufuli katika Kitengo cha Habari na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa mwaka 2020 kwa chama changu mimi na kwa uzoefu wa uongozi, nilikuwa ndio mratibu mkuu hasa mkizingatia kwamba chama chetu mwaka 2020 tulisema tutasimama na Chama cha Mapinduzi katika mgombea wa Urais. Hiyo kazi nilipewa na chama changu na niliifanya kwa uaminifu mkubwa sana; na popote alipo mzee wangu Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mungu ambariki kwa kuendelea kuniamini. Pia nashukuru

chama changu kwa kuniamini kuja hapa katika kugombea hii nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitafanya nini kama kijana niliyechukua jukumu kubwa la kutaka kujitwisha kugombea Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza, mimi kama kijana nimeshiriki katika semina mbalimbali za kimataifa za kuwakilisha vijana nikiwa nimechaguliwa nikiwa bado ni Rais wa Chuo. Niliwakilisha mambo mengi yanayohusu sera za vijana. Tuna sera nyngi za vijana bado haziko *updated*, haziko vizuri. Nikiwa Spika wa Bunge nitajitahidi kuititia sera zinazohusu vijana ili tuone tunaweza vipi kukabiliana na matatizo yanayohusu mambo ya vijana mmoja baada ya mwagine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama Taifa, tunajua tunataka kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo. Nikiwa Spika wa Bunge, nitajitahidi kusimamia sheria na kanuni ili kuhakikisha mambo yote yanaenda katika utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitatoa ushirikiano kwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kujali vyama kwa sababu tupo wote katika kujenga Taifa letu la Tanzania kwa sababu ndiyo mama yetu ambaye tuko naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi la mwisho, nawaomba sana ndugu Wabunge mnipe kura, hasa ukizingatia kama sisi chama chetu tuliweka pembeni mambo ya upinzani wa kuvutana vutana amba hauna faida katika Taifa, tukaamua kusimama nanyi mwaka 2015 na mwaka 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo niko kwenye eneo la nyumbani, sitaki mnitoe na aibu, naombeni kura zenu ili niweze kuwawakilisha. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nawasihi sana kuanzia aliyeo mbele, Waziri Mkuu na Wajumbe wote, naombeni kura zenu ili tuweze kulijenga Taifa hili na tumsaidie mama yetu katika kupiga hatua za maendeleo ya Taifa letu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa la msingi sana, naomba niwatoe hofu kuhusu uzoefu wa uongozi, nina uzoefu wa kutosha sana. Nadhani nyie tu hamjataka kunitumia, lakini uzoefu ninao na nimeongoza taasisi nydingi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa sababu dakika zangu tatu sitaki kuzitumia hadi ziishe, naomba nimalize kwa kusema kwa heshima na taadhima, naomba nipate kura zenu ndugu Wajumbe na Mungu awabariki sana. Tumwombee mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kazi iendelee. Tuko pamoja na vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakaribisha maswali.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa maelezo.

Haya, Waheshimiwa Wabunge, Bwana *Engineer* Aivan Jackson Maganza wa TLP amemaliza maelezo.

Ehe, nimekuona Mheshimiwa Esther.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina swali dogo tu kwa mgombea, *Engineer* Ivan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake ameonesha kwa kiasi kikubwa kwamba chama chake kuitia yeye mwenyewe amekuwa akiunga shughuli nydingi za Chama Cha Mapinduzi na ametueleza kwamba 2020 alichaguliwa kuungana na kampeni ya urais wa Chama Cha Mapinduzi. Sasa swali langu la msingi ni kwamba, amekuaja kugombea nafasi ya Spika na Chama Cha Mapinduzi kina mgombea wa Spika. Ni nini kilichompelea kwa kipindi hiki asiunge kama alivyokuwa akiunga huko nyuma? Ni nini cha

tofauti ambacho amekiona mpaka akaona aje kugombea nafasi ya Uspika kuliko kumwachia mgombea yule? (*Makofii*)

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, okay. Nashukuru sana Ndugu Esther Bulayo... (*Kicheko*)

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: ... Ndugu Esther Matiko...

MWENYEKITI: Mgombea, ngoja basi nikukaribishe. Haya karibu.

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naomba nijiblu swali lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali zuri sana la Mheshimiwa na nimelipenda, la kusema kwamba, kama mimi chama changu kimenitumia muda mrefu kushiriki kazi za Chama cha Mapinduzi, sasa leo Chama cha Mapinduzi kimemsimamisha Dkt. Tulia Hasan kuna haja gani? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Dkt. Tulia Ackson, kuna haja gani mimi kama Chama cha TLP kuja kuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilijibu swali lake kama ifuatavyo:-

(Hapa Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Naomba utulivu Waheshimiwa Wajumbe. Swali lako nalijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini katika njia ya mafanikio wote tunajua tunamtegemea Mungu, natolea mfano mdogo tu, lakini kuna wale wanaoamua kumtumainia huyo huyo Mungu wengine kupitia Msikitini na wengine Kanisani. Kwa hiyo nia yangu kubwa, yale aliyoabeba Tulia

Ackson, mimi niliinadi ilani, Tulia Ackson aliyoabeba, niliinadi ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ninachokijua mimi, yeye ana uwezo wake na mimi nina uwezo wangu kama kijana. Kwa hiyo ninachokitaka ninyi mpime, muone tunamtuma nani akaweze kuwakilisha katika hilo, lakini ninachokisema, kitabu ni kile kile, shida ni unakisoma saa ngapi, asubuhi au mchana. Ahsante sana. (*Makofi/kicheko*)

MWENYEKITI: Haya, swali lingine! Mheshimiwa Papaa Mulugo, Karibu.

MHE. PHILIP A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nina swali moja kwa mgombea. Kwa kuwa wakati akijieleza amejipambanua sana kwamba yeye ni mpenzi sana wa sera za vijana, ingawa humu kuna Waheshimiwa Wabunge vijana, wazee, akinamama na akinababa. Sasa swali langu, nataka anitajle sera tano za vijana za kitaifa na lini zilianzishwa katika nchi yetu ya Tanzania?

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Haya, kama unaweza jibu.

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa sababu na yeye anafuata kanuni amesema hilo si swali, lakini kama naweza nijibu. Naomba tu nimjibu tu kwa kumsaidia pia mjumbe wangu, kwa sababu nategemea atanipigia kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sera ya vijana ambayo Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akiipigia kelele sana kuna mambo mengi sana yanayohusu kuwawezesha vijana kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya kwanza ni kuhakikisha vijana wanapata mafunzo ya msingi ya kuweza kuwafanya wajikimu kwenye maisha yao. Kwenye sera hiyo hiyo ya vijana ukienda kuisoma inasema, vijana watasaidiwa

kupata mikopo ili kuwawezesha kufanya shughuli zao. Sera ya vijana pia inasema itahamisha vijana waweze kuachana na tabia ambazo zinaweza kuwapeka kwenye mazingira hatarishi ili waweze kulijenga Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera nyingine inayohusu vijana ni sera ya vijana inayosema vijana waweze kuhamasishwa ili washiriki kwenye shughuli za Serikali na shughuli zao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la sera ya vijana ni kuhakikisha kuwa vijana wanakuwa walini wa Taifa letu na rasilimali zao, nadhani hizo ndizo sera tano, ukienda kusoma zinapatikana na nadhani Mheshimiwa Rais alishasema lianzishwe Baraza la Vijana, na sisi tunaunga mkono jambo hili litokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana.

MWENYEKITI: Haya, swali la mwisho, naona ameshasimama, karibu sanaMheshimiwa.

MHE. MOHAMED SAID ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwa mgombea, naona katika maelezo yake amejipambanua sana kwenye vijana na humu Bungeni tumo Waheshimiwa Wabunge wa rika tofauti, lakini pia anakuja kuliongoza Bunge ambalo ni taasisi inayoendeshwa kwa mujibu wa Katiba na sheria lakini kwa nchi nzima ya Tanzania ambayo ina kada tofauti ambazo zote zinatakiwa zitungiwe sheria humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; haoni kwamba akiwa Spika atakuwa anasahau sana hizo kada nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, sisi ambao tunataka kumchagua kuwa Spika wetu haoni kwamba atatugombanisha na wananchi ambako huko kuna wazee, kuna walemavu, kuna watoto na kuna kila aina ya rika? Maswali yangu ni hayo.

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri, naomba nijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mjumbe, nadhani maelezo yangu ya awali, kama uliyafuatilia, kwamba tutawawezesha vijana katika kutunga sera, nilisema kwamba nitahakikisha nikiwa Spika wa Bunge, kwa sababu Bunge linaongoza kwa mujibu wa kanuni na sheria, nitahakikisha zile sheria ambazo haziko vizuri kwa ujumla wote tuzifanyie kazi, sasa sikutaka nitaje, maana nigetaja wanawake wazee ningewasahau, nigetaja wazee ningewasahau vijana, nigetaja vijana ningewasahau wenye ulemavu.

Kwa hiyo Bunge letu linandeshwa kwa mujibu wa kanuni na sheria. Kwa hiyo, nikiwa kama Spika wa Bunge nitajitahidi kuhakikisha mambo yote ambayo yanahu Taifa letu tunayaweka sawa.

Kwa hiyo la vijana nimelipachika tu kwa sababu kwa wagombea niliowaona nimeona kama ni vijana na vijana wengi walipoona nimeteuliwa na tume kuja kugombea walikuwa na matumaini makubwa. Kwa hiyo nilitaka kuliweka hilo sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutahakikisha kwamba tutaboresha sera zetu na kuona kwamba, tunasaidiaje kama Taifa kupiga hatua kwenye kutunga kanuni zetu vizuri, kuzisimamia kanuni vizuri pamoja na kuhakikisha kwamba zile kanuni tunazotunga zinaleta matokeo chanya kwa wananchi wetu. Hayo ndio yaliyokuwa maelezo yangu ya awali.

MWENYEKITI: Ahsante sana *Engineer Jackson Maganga* kutoka TLP. Tumemaliza maswali, nafikiri unaweza kuondoka.

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, Mungu awabariki, naombeni kura zenu. Ahsanteni sana. (*Makofii*).

MWENYEKITI: Aingie mgombea wa tatu, Bwana Georges Gabriel Bussungu. *Sorry, mgombea wa tatu ni Bwana David Daud Mwaijojele kutoka CCK.*

(Hapa Ndg. David Daud Mwaijojele Aliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Bwana David Daud Mwaijojele karibu sana. Unagombea nafasi ya Uspika na mbele yako hawa ni wapiga kura. Tutakupa nafasi ya kujieleza dakika tatu, na pia unaweza ukaulizwa maswali matatu kama yapo, karibu.

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina naitwa David Daudi Mwaijojele. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia na kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya waheshimiwa kama ninyi. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wajumbe wote walioko mahali hapa katika mkutano huu mkubwa wa kumchagua Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nawasalimu wote kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hebu tuitikie.

WABUNGE: Kazi iendeleel!

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: itikia kwa nguvu tena, sijasikia.

WABUNGE: Kazi iendeleel!

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Sasa ninyi mnapanga maswali, mimi nataka mrudie hiyo kazi iendeleee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukishukuru chama kilichoniteua katika mchakato uliokuwa kwenye chama. Vilevile niishukuru familia yangu na zaidi Mwenyezi Mungu maana mambo yote yanapangwa na Mungu. Uongozi na kila kitu kinapangwa na Mwenyezi Mungu na si kwa akili za kibinadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mnapiga makofi, hii imewagusa kwa sababu bila Mungu huwezi kitu chochote.

Pia mkumbuke kwamba mnaongea na Mtumishi wa Mungu, Askofu, kwa hiyo nitawahudumia vyote, kwa maelezo, kiroho na kimwili. Mtulie. Maswali hakuna. (*Makof/Kicheko*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa, nafikiri yupo kabisa mbele yangu namuona; Waheshimiwa Wabunge...

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Kanuni zetu za Bunge, hasa unapokuwa humu ndani ya Bunge letu huruhusiwi kusoma. Sasa mgombea wetu tunaona ameweka kabisa gazeti mezani. Sijui taratibu zinasemaje Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnes, huyu si Mbunge. Huyu ni mgombea. Endelea, unaweza ukasoma ama ukaandika kama ndivyo ulivyojiaadaa, endelea.

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu nilikuwa siruhusiwi?

WABUNGE FULANI: Ndiyo!

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Ahaal Mnanirudisha nyuma sasa.

WABUNGE FULANI: Nenda mbele.

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Niendele mbele?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wagombea wenzangu wote wa kiti cha USpika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itifaki imezingatiwa. Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano, tumeshapita hapo, itikia kazi iendelee. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kujitambulisha. Naitwa David Daudi Mwaijolele kutoka Chama cha Kijamii, kwa kifupi ni CCK. Mwanzoni chama hiki kilikuwa kinaitwa Chama cha Jamii. Mara ya pili kikasajiliwa tena kwa Chama cha Kijamii (CCK).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa shukrani na kwa heshima na taadhima nashukuru kwa kuteuliwa kugombea kitu cha Spika wa Bunge la Muungano wa Tanzania.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihusike kusema yafuatayo. Naomba mnichague na kunipatia kura zenu zote zote. Mimi hata sihesabu, hata zikizidi 400 ni sawa tu. Naomba kura za Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili ili tuinue na tukweze mfungamano rafiki wa demokrasia ya mfumo wa vyama vingi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge naomba kura zenu zote na kunichagua niwe Spika wa Bunge hili ili tushirikiane kung'arisha utawala bora na kujenga ustawi na maendeleo ya jamii kiuchumi kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kwa sababu ya muda na niliyo nayo ya kujieleza ni mengi, mkinipitisha kama Spika, ni mengi mno kwa sababu Spika ni lazima awe na *material* mengi. Kwa hiyo naomba kura zenu. Nina uzoefu wa uongozi na nimegombea pia 2020, niliingia kwenye kinyang'anyiro cha kugombea uraisi na 2010 niligombea Jimbo la Kinondoni, 2015 niligombea Ubunge Jimbo la Segerea na 2018 niligombea pia uchaguzi mdogo Jimbo la Kinondoni. Kwa hiyo nimesimama mbele yenu nikiwa mtu mzoefu sana. Msiwe na wasiwasi, mkinichagua kwa hakika nitawahudumia...

MWEYEKITI: Ahsante sana...

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Halafu nitahakikisha kila Mbunge asitoke hapa bila kuongea, aeleze kero za huko jimboni kwake, asikae tu hapa katoka bila kuongea. Mimi ndiye Spika ambaye mnatakiwa muweke rekodi. Mchungaji, kiongozi wa kiroho hakuwahi kuchaguliwa Bungeni, sasa ni nafasi ya kiongozi wa kiroho kuchaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana, naona mnaona nimekiuka kanuni, sijui nimekwendaje! Kazi iendeele.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Bwana David Daud Mwaijojele wa CCK amemaliza kujieleza, endapo kuna Mheshimiwa yejote ana swalii. Karibu Dkt. Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwanza kwa kutambua cheo changu cha Udaktari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumuuliza swalii mgombea. Ameeleza maelezo mengi, lakini mwishoni ameleeza vizuri kwamba amegombea Urais, amegombea Kinondoni na Segerea na kote amefeli. Je, unaitabirije mechii ya leo Mheshimiwa mgombea? (*Kicheko*)

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli swalii la Mheshimiwa Musukuma ni zuri sana. Nimewomba Mwenyezi Mungu awaguse Waheshimiwa Wabunge wote mlioko hapa na uzuri wake tuna Mheshimiwa Waziri Mkuu, huruma ni nydingi, sitatoka hapa bila kupewa kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunatakiwa kufanya kitu cha kuvunja ukanda, udini pamoja na vyama. Hebu nipeni kura zenu bila kuangalia natoka wapi au ni mtu wa namna gani. Nitawafaa sana, nina vitu vizuri sana, mtafurahi Waheshimiwa Wabunge. Mtakaponipitisha tu Mwenyezi Mungu akiwajalia, mkifumba macho mkifumbua, mkitiki tu kwa Mwaijojele, basi mtaona baraka zikimiminika kwa sababu nitakuwa nawaombea na huku naongoza kwa Kanuni za Bunge na Katiba na vitu kama hivyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Swali la pili kama lipo?

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Swali la tatu kama lipo.

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Ndugu David Daudi Mwaijojele maswali yamekwisha, unaweza kuondoka.

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Eee! Mwenyezi Mungu ni mkubwa, mbarikiwe sana. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Aje sasa mgombea wa nne, Bwana Georges Gabriel Bussungu, huyu anatoka Chama cha ADATADEA.

(Hapa Ndg. Georges Gabriel Bussungu Aliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Bwana Georges Gabriel Bussungu karibu kwenye ukumbi huu. Umegombea nafasi ya Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utapewa nafasi ya kujieleza na kuomba kura kwa dakika tatu na unaweza kuulizwa maswali matatu kama yapo, karibu.

NDG. GEORGES GABRIEL BUSSUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WABUNGE FULANI: Kazi iendelee.

NDG. GEORGES GABRIEL BUSSUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WABUNGE FULANI: Kazi iendelee.

NDG. GEORGES GABRIEL BUSSUNGU: Jina langu naitwa Georges Gabriel Bussungu. Nina elimu ya *Degree* ya Uzamili katika masuala ya Biashara. Nimesoma pia *Degree* ya pilii katika Utawala na Uongozi. Nimebobeia katika masuala ya Biashara na Uwekezaji; na pia nimesomea masuala ya uongozi wa kuleta matokeo ya kimkakati. Kutokana na hali hiyo sasa, uzoefu wangu katika Serikali ni miaka 41. Nimefanya kazi katika mikoa mbalimbali na baadhi yenu mnaweza kuona matokeo ambayo nimeyafanya katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa mfano mmoja. Karibu watu wote wanaweza kukumbuka kwamba Singida ilikuwa na hali mbaya sana ya hali ya uchumi, lakini kitu kilicholeta mabadiliko kilikuwa nyuma yangu, ni kutayarisha Mpango wa Kuimarisha zao la Alizeti na kuifanya Singida kuwa bingwa wa Alizeti katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nilikwenda katika Mkoa wa Kigoma, Wabunge wa Kigoma wanaweza wakaona hali ilivyokuwa na mpaka wanamuziki wakaimba Kigoma ya sasa siyo kama ile ya zamani. Hiyo ilikuwa ni nyuma ya mambo yangu niliyoyafanya katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika nilikwenda Manyara na ninashukuru sana nilivyokuwa kule Manyara nilifanya mabadiliko makubwa. Nilikaa muda mfupi sana na nikatengeneza maandiko kadhaa. Andiko moja, nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi amefungua *Tanzanite City*. Hilo ilikuwa andiko langu ambalo nimelifanya kule. Mambo mengine ambayo yamefanya Kitaifa ambayo yamehusiana na masuala ya uwekezaji, bila shaka viongozi wanaweza kuyakumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, nimeweza pia kuiwakilisha nchi Kimataifa katika Mikutano mbalimbali ya Uwekezaji. Nilitoa *Paper* moja kule *Shenzhen University of Special Economic Zone* ya China na kule Shekou kwenye kampuni kubwa sana ya meli ambayo pia ilitaka kuwekeza hapa nchini. Pia nimehudhuria mkutano na kutoa mada kule Malaysia kwenye masuala ya Uwekezaji wa Kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mambo kama hayo ya uwekezaji na mambo ya kimatokeo, inaonesha wazi kwamba naweza kufanya kazi vizuri nanyi tukishirikiana ili kuleta mabadiliko katika Bunge. Kwa sababu sisi wote humu ndani Waheshimiwa Wabunge ni wanamapinduzi (*revolutionized*) tunataka tuwe na mabadiliko, kwa sababu nchi sasa iko kwenye vita vikubwa sana vya kiuchumi, kwa hiyo, inahitajika kiongozi awe katika mtazamo mpana wa kiuchumi ili kuweza kusaidia Bunge kuweza kuisimamia vizuri zaidi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mgombea kujieleza)

NDG. GEORGES GABRIEL BUSSUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana kwa kweli kupata fursa hii naomba mnichague kwa mantiki hiyo kwamba mnapata mtu ambaye ataweba kuleta teknolojia mpya na kulifanya Bunge liwe la kisasa zaidi na kuleta mabadiliko ambayo Mheshimiwa Rais wetu anayatarajia.

Imani ya Mwenyezi Mungu iwabariki nyote na ninaomba mnipe kura za wingi ili niweze kufanikisha azma ya Taifa la Tanzania. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Ndugu Georges. Waheshimiwa Wabunge, mgombea amemaliza kujieleza. Kama kuna swalii; swalii la kwanza!

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Swalii la pili?

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Swalii la tatu.

WABUNGE FULANI: Ndugu Georges.

NDG. GEORGES GABRIEL BUSSUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Naombeni kwa heshima na taadhima, kwa kuzingatia tai hii, kwa kweli mnichague niwe Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Kicheko/Makofi*)

Ahsanteni sana. (*Makofi*)

(*Hapa Ndg. Georges Gabriel Bussungu Aliondoka Ukumbini*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Aingie sasa Bwana Kunje Ngombale Mwiru. Huyu ni Mgombea wa *SAU*.

(*Hapa Ndg. Kunje Ngombale Mwiru Aliingia Ukumbini*)

MWENYEKITI: Bwana Kunje Ngombale Mwiru anatoka Chama cha *SAU*, anagombea nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mbele yako ni wapiga kura ambao ni Waheshimiwa Wabunge, utapewa nafasi ya kujieleza kwa dakika tatu na utaulizwa maswali matatu kama yatakuwepo. Karibu sana Ndugu Kunje Ngombale Mwiru.

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nawashukuru sana ndugu zangu Wabunge, nawashukuru sana Mawaziri kwa kuwa nanyi leo kwa siku ya leo ambayo ni siku muhimu sana ya kumchagua Spika wa Bunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina naitwa Kunje Ngombale Mwiru, ni mwanasiasa wa muda mrefu, nipo katika vyama mbalimbali; nilikuwepo CHADEMA, nikaenda ACT, na sasa nipo Sauti ya Umma (*SAU*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa baraka niliyopewa na familia yangu ya Ngomale Mwiru, wamenipa ridhaa ya kuja hapa kuomba kura kwenu kutaka kupata nafasi ya

kugombea Urais, kugombea Ubunge, kugombea Uspika...
(Makof)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wageni wote Waalikwa, vyombo via dola, vyombo via dini, nawaombeni mimi Kunje Ngombale Mwiru; nimekuwa kiongozi wa vyama via siasa. Kwa sasa hivi nipo Chama cha Sauti ya Umma (SAU) kama Mwenezi wa Mambo ya Siasa na nimekuwepo kwenye Shirika la Tiba Asilia na Utunzaji wa Mazingira (*TRAMEPRO*) nimekuwa mtu ambaye nimehubiri katika shirika lile kwa muda mrefu kwa ajili ya kupingana na imani potofu ya waganga wa kienyeji ili kupunguza mauaji kwa njia ya ushirikina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya hivyo kwa sababu moja, nilikuwa na mzee wangu katika shirika lile, Mheshimiwa Marehemu wetu Kingunge Ngombale Mwiru, nilikuwa naye kwenye shirika lile kwa muda mrefu sana. Naye aliteuliwa wakati akiwa hai, kuja katika Bunge hili la Katiba kuja kuzungumzia masuala ya tiba asilia na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombeni sana ndugu zangu Wabunge, nimekuja kwenu leo mniipe ridhaa ya kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani nitalitendea haki Bunge hili na nitatoa changamoto zote zilizokuwemo ndani ya Bunge hili na kuliweka Bunge liwe na mfano duniani na Afrika kwa ujumla.

Ndugu zangu Wabunge mtegemee mafanikio makubwa sana kuptitia kwangu, kwani nitaondoa zile changamoto zilizokuwepo za Wabunge kudaiwa vile vyombo via usafiri wakati wanaenda kufanya kazi kuwatumikia wananchi. Nitaondoa madeni yote. *(Makof)*

Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge mtegemee kabisa, mkinipa ridhaa leo mkanichagua hapa mkanipa kura za kutosha...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mgombea kujieleza)

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajitahidi sana kusimamia haki za msingi za Bunge na nitatenda haki kwa kila Mbunge. Kama nilivyowaambia, narudia tena; Watanzania wanahitaji mafanikio kupitia kwa Wabunge wao. Kwa hiyo, nitajitahidi kuondoa kabisa changamoto za Wabunge. Wabunge wanatakiwa wawe na nyuso za furaha ili wananchi wao waweze kupata mafanikio. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni tajiri...

MWENYEKITI: Muda umekwisha.

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sana kwa heshima na taadhima, nipo mbele yenu hapa, mimi ni kijana wenu, naomba katika hizo kura zitakazopatikana; na tena napenda kuwaomba viongozi wenzangu, Wabunge vyama vya upinzani, wakiongozwa na Mheshimiwa Halima Mdee popote ulipo, naomba unichague mimi niwe Spika wa Bunge hili ili tuweze kufanya Bunge hili liwe la mfano kwa Afrika na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mpinzani wa kweli na ndio maana nimetembea vyama vingi, najua sifa za wanasiasa.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana. Naombeni kura zenu Waheshimiwa.

MWENYEKITI: Haya, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, Ndugu Kunje Ngombale Mwiru amemaliza kujieleza, sasa tunayo nafasi ya kuuliza maswali.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Swali swali.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Jacqueline.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kumwuliza swali Mgombea, Ndugu Ngombale Mwiru. Ndg. Ngombale Mwiru ameonyesha uzoefu wake kwa namna ambavyo amekuwa hakihamahama vyama. Ameeleza hapa kwamba ana zaidi ya vyama vitano amehamahama. Hii inaonyesha wazi kwamba hana msimamo katika kuijunga na vyama, lakini pia katika kusimama kwenye vyama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, swali langu ni kwamba, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linahitaji kuongozwa na kiongozi mahiri, kiongozi ambaye atakuwa na msimamo, hekima na burasa, asiyeyumbishwa yumbishwa kama ambavyo yeye amekuwa akiyumbayumba kama mawimbi ya baharini: Je, atatudhibitishiaje Bunge hili leo kwamba akichaguliwa atakuwa ni kiongozi ambaye atakuwa na msimamo na kuacha tabia hiyo ya kuyumbayumba kama mawimbi?

MWENYEKITI: Hilo siyo swali, kwa sababu kwenda vyama ni utashi na Katiba zetu zinaruhusu; lakini bwana Kingunge kama unataka kujibu unaweza kujibu. (*Makof*)

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali lake lakini nataka nimdhibitishie Mheshimiwa kwamba kuhama hama vyama iko ndani ya Taifa letu na ndani ya nchi yetu.

Kwa hiyo, mkinipa Uspika, siwezi kuhama kwenda kuwa Spika na kuongoza Bunge la Uganda. Nitaendelea kuwepo hapa hapa. Ahsanteni sana. (*Makof/kicheko*)

MWENYEKITI: Haya, swali la pili. Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa mujibu wa maelezo ya mgombea, Ndugu Ngombale Mwiru, amesema kwamba yuko tayari, yaani atakapopata nafasi ya kuwa Spika kutatua changamoto mbalimbali zinazohusu Bunge. Sasa naomba aeleze changamoto tatu zinazohusiana na *functions* tatu za Bunge la Tanzania na namna gani atazitattua?

MWENYEKITI: Endelea.

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Changamoto tatu ulizohitaji; ya kwanza kabisa, naomba nikujibu maswali yako mazuri uliyoniuliza. Changamoto za Waheshimiwa Wabunge, nadhani ninyi wenyewe mnafahamu, kwa sababu miundombinu ya vijiji na vitongoji kuna milima mirefu na mikubwa. Kwa hiyo, kama Mbunge, anatakiwa akabidhiwe gari lenye hadhi, lenye kupanda milima mirefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkinichagua kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitahakikisha kila Mbunge lazima namkabidhi gari lenye uhakika bila mkopo. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge nchi yetu imejaaliwa, hatuna sababu ya kupeana madeni kwa sababu Mbunge ukiwa na madeni ya kulipa gari utashindwa kuwasaidia Watanzania ambao wanahitaji maendeleo kutoka kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili kwa Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu masuala ya vikao. Vikao vimeduwa vingi, tunahitaji vikao viwe vichache lakini nitaongeza posho. (*Kicheko/Makof*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Tafadhali Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Naomba tusikilizane *please!* Waheshimiwa Wabunge, tunyamaze kidogo amalizie. Haya, nakupa nafasi uendelee.

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekeiti, narudia tena, msimamo wangu ni huo huo mmoja. Nitapunguza idadi ya vikao, nitaongeza posho ili mwende vijijini mkawasaidie Watanzania. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Haya swali la tatu.

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekeiti, naomba kumalizia changamoto ya tatu. Sisi Wabunge tunahitaji tuwasaidie Watanzania. Kuna mambo mengi tunayafanya, lakini wapo Wabunge ambao Majimboni kwao hawaonekani. Kwa hiyo, mkinipa Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, nitaanzisha Kitengo cha *Task force* cha kumfuatilia Mbunge mmoja mmoja... (*Kicheko/Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekeiti na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. Kutokana na muda wangu wa dakika tatu na tena nimepitiliza, naomba unisamehe.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Swali la mwisho...

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekeiti, naomba mniruhusu, naombeni mnipe kura zenu ili tuweze kulisogeza mbele Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsanteni sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa George Mwenisongole nimekuona.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Mwenyekeiti, ahsante kwa kunipa hii nafasi.

(Hapa kipaza sauti kilizimika)

MWENYEKITI: Nafikiri kuna *microphone* nyingine imefunguliwa huko. Haya.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa hii nafasi.

Ndugu Mgombiea, kwa kweli umetufurahisha, kidogo unanishawishi nikupe kura, lakini napenda nifahamu msimamo wako ukiwa Spika. Nini msimamo wako wa nchi kukopa ukiwa kama Spika?

MWENYEKITI: Jamani hilo swali linahusiana na mgombiea?

WABUNGE FULANI: Hapana.

MWENYEKITI: Haya, Wapiga kura wamesema hilo siyo swali.

WABUNGE FULANI: Swali!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bwana Kunje Ngombale Mwiru, maswali matatu yamekwisha. Unaweza kuelekea kule ulikokuwa. (*Makof!*)

(Hapa Nd. Kunje Ngombale Mwiru Aliondoka Ukumbini)

MWENYEKITI: Aingie sasa mgombiea wa sita Bi. Maimuna Saidi Kassim huyo anatoka Chama cha ADC. Bi Maimuna Saidi Kassim.

(Hapa Nd. Maimuna Saidi Kassim) Aliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Bi. Maimuna Said Kassim, umeomba nafasi hii ya Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mbele yako hapa ni wapigakura ambaao ni Wabunge wa Bunge hili, tunakupa nafasi ya kujieleza na kuomba kura kwa dakika tatu na unaweza ukaulizwa maswali matatu kama yapo. Karibu sana Bi. Maimuna.

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Kwanza kabisa nianze kwa kuwasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WABUNGE FULANI: Kazi iendelee.

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku hii ya leo na niwashukuru viongozi wangu wa Chama cha *Alliance for Democratic Change* kwa kuweza kunteua ili kuweza kugombea nafasi hii ya Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina naitwa Maimuna Said Kassim, nina umri wa miaka 21, samahani nina umri wa miaka 27, ni mke na ni mama mwenye mtoto mmoja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu matarajio yenu na matarajio ya Watanzania kwa ujumla tukiongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Matarajio yenyе msingi wa kuleta maendeleo chanya kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio haya hayawezi kufikiwa endapo hakuna umoja na mshikamano katika Taifa letu. Hivyo, naombeni kura zenu ili niweze kuhakikisha tunashikamana na tunakuwa wamoja ili kwenda kutetea maslahi ya wananchi kwa kuweka itikadi zetu za vyama pembeni na kusimama wamoja kwa kutoa hoja zenye tija kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana, naombeni kura zenu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ndugu Maimuna Said Kassim amemaliza maelezo, nawauliza Waheshimiwa Wabunge kama kuna mtu mwenye swali. Haya, swali la kwanza Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mgombea amesema anajua matarajio yetu kama Wabunge ya aina ya Spika tunayemtaka, lakini na Watanzania. Napenda anitajie matarajio matano kutoka kwa Wabunge na ameyapata wapi kwa sababu mimi pia ni mpigakura; amejuaje matarajio yangu? Kwa hiyo ninataka pamoja na mengine, atutajie matano ambayo ni matarajio yetu kwa aina ya Spika tunayemtaka.

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa swali zuri Mheshimiwa. Kwanza kabisa nianze kwa kuomba kura yako ya ndiyo ili niweze kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, pili, tarajio kubwa la sisi vlongozi na Watanzania ni kuhakikisha tunapata maendeleo chanya kwa ajili ya Taifa letu; hilo ndiyo tarajio kubwa. Tupo hapa tukiwa tumetokea katika vyama mbalimbali lakini wananchi wametuweka tuweze kusimama pamoja na kuhakikisha kuwa tunatetea maslahi yao. Hilo ndilo tarajio kubwa la sisi Watanzania. Nashukuru.

MWENYEKITI: Swali la pili? Mheshimiwa Malembeka.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali. Napenda kumuuliza swali mgombea, Bi. Maimuna; pamoja na kazi nydingi za Spika, ni lazima awe na kumbukumbu nzuri kwa sababu humu ndani tuna Wabunge zaidi ya 300 na wote awajue kwa majina yao. Yeye wakati anajitambulisha ametaja ana miaka 21, halafu akasema ana miaka 27; sasa nataka njue, umri wake wa ukweli ni upi? Ahsante.

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali zuri Mheshimiwa. Ndugu zangu mimi ni binadamu kama binadamu mwingine, binadamu tunateleza, tunakosea. Umri wangu mimi ni miaka 27, nimezaliwa mwaka 1994, mwezi Aprili, tarehe 16. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paulina, aliwahi kabla ya wengine.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumuuliza mgombea, Ndugu Maimuna, swali lifuatato; Ndugu Maimuna, hii nafasi ya Spika ni nafasi kubwa, ni mhimili muhimu sana katika Taifa letu, lakini naomba kukuuliza; je, una uzoefu wa namna gani katika masuala ya uongozi? Tungependa kujua, lakini pia tunapenda kujua elimu yako ili tuone je, inaweza kutuongoza Bunge letu kwa uhakika zaidi? Ahsante.

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika suala zima la taaluma nina Shahada katika masuala ya Sayansi ya Siasa, Utawala na Utumishi wa Umma nilioipata katika Chuo Kikuu cha Dodoma mnamo mwaka 2018. Vilevile nina Astashahada katika masuala mazima ya *Shipping and Port Management* ambayo nimeipata katika Chuo cha Bandari mnamo mwaka 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala mazima ya uzoefu katika uongozi na siasa, nina uzoefu ndugu zangu. Kwanza, nilikuwa Mbunge katika Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Vilevile nilikuwa Waziri wa Habari na Mawasiliano kuanzia mwaka 2017 hadi mwaka 2018. Vilevile, katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nilifanikiwa kugombea nafasi ya Ubunge katika Jimbo la Kilindi liliopo Mkoani Tanga na niliweza kufanikiwa kupata kura zaidi ya 18,000 na kuweza kupata nafasi ya pili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naombeni kura zenu za ndiyo kwa wingi ili tuhakikishe Bunge letu linakuwa imara na kuweza kutetea maslahi ya wananchi kwa pamoja. Kumbukeni ndugu zangu, niko hapa kuomba kura ya kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na siyo kuwa Spika wa chama chochote cha siasa, hivyo, naombeni kura zenu kwa wingi. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Bi. Maimuna Said Kassim. Maswali matatu yamekwisha, tunakuruhusu.

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(Hapa Ndg. Maimuna Said Kassi Aliondoka Ukumbini)

MWENYEKITI: Aingie sasa Bwana Ndonge Saidi Ndonge wa Chama cha AAFP.

(Hapa Ndg. Ndonge Saidi Ndonge Aliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Ndugu Ndonde Saidi Ndonde, unagombea nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mbele yako ni wapigakura amba ni Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hilli, unapewa nafasi ya dakika tatu kujieleza na unaweza ukaulizwa maswali matatu kama yatakuwepo; karibu.

NDG. NDONGE SAIDI NDONGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naona miwani yako kidogo haioni vizuri, naitwa Ndonge Saidi Ndonge, niweke sawasawa hilo, lakini nashukuru.

Waheshimiwa Wabunge, *Asalaam aleykum*, amani ya bwana iwe juu yenu. Kwa jina naitwa Ndonge Said Ndonge, natokea Chama cha AAFP na nipo mbele yenu leo kwa dakika hizi tatu nilizopewa kuwashawishi au kuomba ridhaa yenu ili niwe Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo niweke sawa kidogo kwamba mimi kwa falsafa yangu sipendi sana kuitwa mgombea kwa sababu ukiitwa mgombea maana yake kuna ugomvi na watu amba wako vizuri hawawezi kugombana kwa sababu kugombana maana yake ni kufuata kitu bila utaratibu. Kwa hiyo napenda nianze kushauri Serikali hata kwenye chaguzi mbalimbali basi liondolewe neno mgombea liwekwe mwomba ridhaa, iwe mwomba

ridhaa wa kiti cha Uenyekiti wa Mtaa, muomba ridhaa wa kiti cha Udiwani, na hata mimi hapa ni muomba ridhaa wa Kiti cha Uspika kupitia Chama cha AAFP.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sasa hivi tupo *next level*, yaani tupo hali ya juu sana kwenye siasa hatuwezi tukaanza kutumia neno mgombea. Ndiyo maana wengine huwa wanakwenda hadi mahakamani, wanapigana, kwa sababu ya neno mgombea, ukitilafsiri maana yake hakutakuwa na usalama. Nilitaka niweke hilo sawa na naamini watu wa Kiswahili wataongea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu, nimekuja hapa leo na kwa sababu ni mara ya kwanza kusimama eneo hili na naamini nitasimama tena baada ya kuapishwa hapo punde, mimi niseme natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan maana yake mpaka sasa hivi vijana wanasema anaupiga mwangi kwa sababu, hili niseme kidogo, kwamba kwa sababu sisi watu ambao tuna mengi ya kusema hatuna nafasi ya kusema na waliokuwa na nafasi ya kusema hawana la kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama kaupiga mwangi sana kwenye madarasa, sana. Zamani kulikuwa na chaguzi karibu nne za kwenda *form one*; kuna chaguzi ya mwezi Januari, kuna chaguzi ya mwezi Machi. Wakati mwagine mtu mlisaozesha mwezi Mei unaletewa barua kachaguliwa huyu awamu ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku jamaa anampigia mkwewe kumuuliza kama aliyemwozesha kashapata ujauzito, kama hajapata basi huku kimeumana, kafaulu. (*Kicheko*)

Kwa hiyo watu wanaulizana pale fomu ya shule anunue baba mkwe au mume, lakini mama hiyo kaiondoa tarehe 17 Januari vijana wote wamekwenda shule tena shule madarasa ya maana; hilo nimsifu sana mama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia madarasa kapeleka mpaka Kawe, madarasa ya *Covid* yamekwenda mpaka Kawe. Mama bwana mama mtu. Hivi hivi tu Kawe yasingekwenda madarasa lakini mama hana hiyana, mama hongera sana, nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa wananchi wa Tanzania, mimi leo nimesimama hapa kwa jambo moja dogo sana; Bunge hili ni Bunge imara, Bunge hili ni Bunge lenye heshima kubwa, la maendeleo...

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

NDG. NDONGE SAIDI NDONGE: ...ni Bunge kati ya Mabunge ambayo yana sifa Afrika na duniani, lakini Waheshimiwa Wabunge ninyi mnajua, wote hapa tupo kwa ajili ya maendeleo na tunapofanya maendeleo lazima tufanye mabadiliko. Kutakuwa siyo kweli kama unasema unafanya maendeleo, yaani unahitaji maendeleo, lakini unafanya vitu vilevile. Maendeleo yanakuja na mabadiliko na mabadiliko ni lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mzee wangu, sasa hivi tunamuita mzee wa Msoga, aliyahi kusema usipobadilika mabadiliko yatakubadilisha, tusifikie huko. Ujanja ni kuchanja, ujanja ni kubadilika. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafikaje kwenye maendeleo, lazima tuanze na mabadiliko na mabadiliko hayo ni yapi ili twende kwenye maendeleo? Mabadiliko hayo yapo kwenye mikono yenu na kwenye vichinjio yenu. Kama ingekuwa kule mtaani tungeita kwenye vichinjio, kama ingekuwa uchaguzi wa nje, lakini hapa tunasema yapo kwenye mikono yenu na maendeleo hayo ya kufanya ni kumfanya muomba ridhaa anayegombea hapa mbele, Bw. Ndonge Said Ndonge, kuwa msimamizi wa Mhimili huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, tuanzie hapo. Tukianzia hapo basi maendeleo yatakuja kwa sababu itakuwa tayari tumeanza kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama watu wote tupo tayari kwa ajili ya maendeleo basi tuanze kubadilika. Mnipe kura zenu zote za ndiyo, mwisho wa siku niende na mimi niseme kwa sababu tu nimekuwa wa saba hapa, lakini kama inawezekana, kwa hotuba yangu hii fupi basi ningewaomba hata wagombea wenzangu watangaze kujitoa ili kazi iwe rahisi zaidi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemaliza.

MWENYEKITI: Ahsante sana Ndugu Ndonge Said Ndonge. Haya, Mheshimiwa Bwana Ndonge Saidi Ndonge amemaliza; kuna mtu ana swali?

Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa wajibu wetu ni kufuatilia taratibu zote zinavyokwenda vizuri ili uchaguzi wetu ufike mpaka mwisho salama, sasa niliona ndugu mgombea kama akipokea kitu na kuweka mfukoni, sikuelewa ni kitu gani. Kwa hiyo napenda kufahamu tu kama ni kitu cha kawaida ili kama ni kitu kidogo cha kawaida basi anaweza akaisema wazi ili isituletee shida, kwa ajili ya masuala ya kiuadilifu.

MWENYEKITI: Haya, nadhani hilo siyo swali. Yupo Mheshimiwa Mbunge mmoja baada ya maelezo ya Ndugu Ndonge Saidi Ndonge ambayo wote tumekubali hapa kwamba Mama ameupiga mwingu; na amefafanua vizuri, kwamba zile *stages* za usaili wa wanafunzi mwaka huu kwa mara ya kwanza wanafunzi wote wamesailliwa mara moja. Sasa amefurahia tu, ingekuwa huyu ndio amesimama kwenda kumpa yule, tungenesema rushwa, lakini yule kampa huyu. Kwa hiyo, ni jambo la kawaida, amefurahi. (*Makof*)

Swali la pili, naomba mwenye maswali.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Taarifa! Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Getere, swali la pili.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kikao cha leo.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: ...na Mungu aendelee kukubariki hapo ulipo na uendelee kubarikiwa.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mgombea umeeleza mambo mazuri sana. Sasa katika Bunge hili unalogombea kuwa Spika kuna mihimili mitatu; kuna Bunge lenyewe, kuna Serikali ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Mama Samia na kuna Mahakama. Sasa ukiwa Spika wa Bunge hili, utashirikianaje na mihimili miwili ambayo imebaki na hasa muhimili wa Serikali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bwana Ndonge Saidi Ndonge, endelea.

NDG. NDONGE SAIDI NDONGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama alinisikia Mheshimiwa Mbunge, najua kila mtu unatakiwa umfanyie kile anachokipenda eh. Nilisema usiniite mgombea, niite mwomba ridhaa. Nasemaje kwenye jibu lako? Wewe kwanza nichague, halafu uone shughuli. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Haya, swali la tatu na la mwisho.

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Swali la tatu!

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Swali la tatu!

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Ndugu Ndonge Saidi Ndonge, wamekufurahia sana watu kwa meseji uliyoitoa. Maelezo yako nafikiri umemaliza na maswali yameisha. Tunakushukuru sana. Tunakuruhusu.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Labda, hebu subiri kidogo Mheshimiwa Ndonge. Utaratibu unamhusu huyu?

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unamhusu.

MWENYEKITI: Ehe!

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Kwa kuwa amezungumza vizuri na wewe umetolea ufanuzi, nami nataka kumwongeza lakini niweke na neno kidogo, kwamba kwa sababu sio Mbunge, anaomba ridhaa kama alivyosema; hata sisi Wabunge tunapokwenda kuzungumza kwenye mikutano, ukizungumza maneno mazuri yanayowagusa wananchi, tunapewa mpaka jogoo. Kwa hiyo, hiki siyo kitu cha ajabu. Kuna... (*Makofii/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, unaweza kwenda. Ahsante sana. (*Makofii/Kicheko*)

(Hapa Ndg. Ndonge Saidi Ndonge Aliondoka Ukumbini)

(Hapa baadhi ya Wabunge walimtzanza fedha Mgombea wa nafasi ya Spika, Ndg. Ndonge Saidi Ndonge)

MWENYEKITI: Haya, enhee! Naona maneno ya Bwana Ndonge yamewagusa sana Waheshimiwa Wabunge. Haya, na Mbunge wa Kawe anasema madarasa yamefika. Ahsante

sana. Mnaweza kuendelea kumchangia huko nje. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Mama Mtu! (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaomba utulivu! Tunaomba utulivu! Hii ndio Tanzania ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita angependa kujenga, Tanzania ambayo maneno kama haya yanaweza yakatoka kwa mpinzani. Zamani tulizoea watu kupinga kila kitu, lakini leo tunaelewana, tunajenga nchi moja. (*Makofi/Kicheko*)

Aingie sasa Bwana Saidun Abdulrahman Khatibu kutoka Chama cha DP.

(Hapa Ndg. Saidoun Abdulrahmani Khatibu Aliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Bwana Saidoun Abdulrahmani Khatibu, umeomba nafasi ya Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mbele yako ni wapiga kura ambao ni Wabunge wa Bunge hili. Nakupa dakika tatu za kutoa maelezo na kuomba kura na baada ya hapo unaweza ukaulizwa maswali matatu na Wajumbe hawa kama yapo. Karibu.

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla ya kuongea kitu chochote, jina langu siyo Saidoun. jina langu naitwa Saadun Abdulrahman Khatibu; 'i' iondoke. Jina langu ni Saadun Abdulrahman Khatib.

MWENYEKITI: Endelea.

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Asalaam Aleykum.*

WABUNGE FULANI: *Waaleykum Salaam.*

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwana Yesu Asifiwe.

WABUNGE FULANI: Amen.

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Nawasalimu kwa Salamu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WABUNGE FULANI: Kazi iendelee.

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mnayeniona hapa ni mgombea kupitia tiketi ya DP (*Democratic Party*). Jina langu naitwa Saadun Abdulrahman Khatibu, ni Mtanzania, ninayetokea visiwa vya Zanzibar. Nimezallwa Pemba, Mkoa wa Kusini Pemba, Wilaya ya Kusini Pemba, Jimbo la Chambani. Nia yangu ya kugombea nafasi ya Uspika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kwa sababu Kiti cha Uspika kipo wazi kisheria. (Makofii)

Ndugu Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja anajua kwamba matarajio yake anahitaji kitu gani? Anahitaji uhuru na haki katika kusimamia majukumu ya Uspika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Bunge.

Ndugu Wabunge, nami matarajio hayo nawahakikishieni mkinichagua kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania nitakuwa mtu wa kwanza nitakayeongoza kwa haki na huru, mfurahie kiongozi wenu mpya wa Uspika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nini nikasema hivyo? Kwa sababu ninazo sifa za kuwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Ndugu Wabunge, kwa hiyo, naomba mnichague kwa kura nydingi kwa sababu ninazo sifa za kuwa Kiongozi Mkuu (Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naelewa nikiweza kufanya kazi kwa uadilifu, huru na haki, kwa upendo na huruma kwa mujibu wa sheria za nchi, basi naamini mtafurahia nafasi hiyo. Kwa hiyo, nawahakikishieni kwamba kiongozi mzuri ni yule tu anayependa kutawala nyoyo za watu; na kiongozi mzuri sio yule anayetawala viwiliwili nya watu. Nami ni mmoja ambaye napenda kuongoza kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Juu ya Bunge hili Tukufu, nitalifanya haki na uadilifu. Naomba kura zenu za ndiyo ili niweze kusimamia majukumu yangu.

Ndugu Wabunge, nimesimama mbele yenu kwa unyenyekevu na heshima na taadhima kuomba kura zenu za ndiyo za kutosha niweze kusimama pamoja ili kuweza kufanikisha azma yetu ya kusimama kama viongozi katika Uspika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni.

MWENYEKITI: Ahsante sana Bwana Saadun Abdulrahman Khatibu. Nafikiri nimelitamka vizuri jina lako, Saadun Abdulrahaman Khatibu.

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Ndiyo.

MWENYEKITI: Amemaliza kujieleza. Kama kuna mtu ana swali, swali la Kwanza.

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Swali la pili.

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Swali la tatu.

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MWENYEKITI: Ndugu Mgombea maswali hakuna.

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Ahsante, nashukuru ndugu Wabunge.

MWENYEKITI: Ahsante.

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Ahsante sana.

(Hapa Ndg. Saidoun Abdulrahman Khatibu Aliondoka Ukumbini)

MWENYEKITI: Anayefuata, sasa kujieleza wa mwisho lakini siyo kwa umuhimu ila kwa mpangillo tu, anaingia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mgombea wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Vigelegele)*

(Hapa Mhe. Dkt. Tulia Ackson Aliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Ndugu Mgombea, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, umegombea nafasi ya Ubunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. mbele yako kuna wapiga kura ambaao ni waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili. Nakupatia dakika tatu za kujieleza na kuomba kura na Waheshimiwa hawa ambaao ndio wapiga kura wanaweza wakakuuliza maswali matatu kama yapo. Karibu.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ambayo nimeipata mbele ya Bunge hili tukufu niweze kuomba kura na ridhaa yao ili niweze kuwa kiongozi wa mhimili huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu naitwa Tulia Ackson, nami kama Wagombea wengine nimekuja ili niombi ridhaa yenu Waheshimiwa Wabunge ili katika kuhakikisha Taifa letu linapata maendeleo, basi mimi niwe nawaongoza halafu wote tunakwenda kwa pamoja kama Wabunge.

Pengine kinachonitofautisha na wagombea wengine ni kwamba mimi ni Mbunge mwenzenu. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba ridhaa hii nikiwa natambua kazi kubwa ya Bunge lakini pia kazi kubwa ya hayo mamlaka ambayo ninyi kama mtanipa ridhaa siku ya leo nitakuwa nayo. Sasa kwa sababu nimepewa dakika tatu, sisi kama Wabunge kazi yetu kubwa ni kuishauri na kuisimamia Serikali, kuhakikisha inapeleka maendeleo kwa wananchi. Kazi kubwa ya Spika ni kuliongoza Bunge katika majukumu hayo ambayo Bunge limepewa Kikatiba.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mkinipa ridhaa ya kuwa Spika wa Bunge hili, nitaliongoza Bunge hili kwa mukhtadha huo wa kuhakikisha Waheshimiwa Wabunge mnapata fursa ya kuihoji Serikali kwa heshima na kwa busara na kufuata kanuni zetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia mtapata fursa ya kutumia haki yenu ya kuwawakilisha wananchi, kuleta hoja zenu mbele ya Serikali; na ili Serikali iweze kuangalia vipaumbele inavyoweka, lazima isikilize wananchi wanasema nini; nanyi ndio wawakilishi wa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uwakilishi wenu huo, basi kazi kubwa kwangu mimi mkinipa ridhaa itakuwa ni kuwapa fursa ya kutoa mawazo yenu ambayo mtakuwa mmeyatoa kwa wananchi kwa sababu Bunge kimsingi ni daraja kati ya wananchi na Serikali. Kwa hiyo, Serikali; na hapa tunaongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, yeye ni sehemu yetu kwa sababu ni kazi yake kufahamu wananchi wanasema nini, naye akishasikia humu ndani, basi anajua kwamba Wabunge wameleta mawazo ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa machache hayo na muda wangu umekwisha, naomba kura zenu Waheshimiwa Wabunge ili nipate ridhaa ya kuwa Kiongozi wenu ambaye

tumeshafanya kazi wote kwa muda kidogo, kwa hiyo, tunafahamiana.

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, mgombea wa Chama cha Mapinduzi. Waheshimiwa mnayo nafasi ya maswali.

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwulize

MWENYEKITI: Swali la kwanza atauliza Mheshimiwa Mrisho Gambo halafu atakuja Mheshimiwa Aida.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Bunge hili lina Wabunge wengi wa CCM na wananchi wanaamini kwamba ni rahisi Wabunge kumezwa na Serikali na hivyo kushindwa kuikosoa na kuisimamia Serikali: Swali langu ni: Je, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson tukikuchagua kuwa Spika, unatuhakikishiaje kulinda heshima na hadhi ya Bunge ndani na nje ya Bunge hili? (*Makof*)

MWENYEKITI: Karibu Mheshimiwa Dkt. Tulia.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nilijibu swali hili kwa muktadha wa majukumu yetu sisi kama Wabunge, kama mhimili ambao umepewa kazi Kikatiba wa kuisimamia na kuishauri Serikali. Hailishi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi wa Chama cha Upinzani, anapoleta hoja humu ndani, yeye ni mwakilishi wa wananchi.

Sasa kwenye hoja kwamba Bunge kwa sababu lina Wabunge wengi wa Chama cha CCM, linaweza likamezwa na upande wa Serikali, huo uwezekano haupo kwa sababu Serikali haiwezi kulimeza Bunge na wala Bunge haliwezi kumezwa na Serikali. Kwa sababu Katiba yetu imeweka majukumu tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kazi yake ni utendaji, Bunge kazi yake ni kuisimamia Serikali kuhakikisha je, kutenda kwake inaleta maendeleo kwa wananchi au hapana. Ndiyo maana Mwenyekiti wetu wakati akifungua kikao hiki ameeleza namna ambavyo maendeleo yanapelekwa nchi nzima kwenye majimbo yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unapopeleka hayo maendeleo huko kwa wananchi, sisi tukiwa hapa na wananchi watapata fursa katika wiki hizi tatu za Bunge hili kuona namna ambavyo Serikali hii imefanya kazi kwenye Majimbo na pia Serikali itasikia namna ambavyo pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali changamoto zipo, watawasikia Wabunge wakiuliza maswali, watawasikia Wabunge wakizisema hoja hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia kama Mbunge wa Mbeya Mjini, wananchi wa Mbeya Mjini watasikia changamoto zao zikisemewa humu Bunge. Kwa hiyo, uwezekano wa Wabunge kushindwa kufanya kazi yake, kwa sababu pengine Wabunge wengi ni wa Chama cha Mapinduzi haupo, kwa sababu wananchi waliwachagua hawa Wabunge siyo kwa ujumla wao, kila Mbunge alichaguliwa kwenye Jimbo lake kwa uwezo wake wa kuwaongoza wananchi ambao walimpa ridhaa hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa fursa hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru. Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nitanukuu maelezo machache ambayo ameyasema Dkt. Tulia Ackson Mwansasu. Amesema kazi ya Bunge ni kushauri na kuisimamia Serikali, sura iliyoko huko nje kama unavyojuua hili Bunge tuko sisi wachache tukichukua mawazo ya wananchi. Sura iliyoko nje pamoja na kwamba Serikali yetu inaongozwa na mihimili mitatu ikiwepo Bunge, kushirikiana mihimili mitatu kupeleka

maendeleo kwa Watanzania si jambo baya. Jambo baya linakuja inapotokea mhimili mmoja kuingilia kwenye mhimili mwingine na wewe umekuwa Naibu Spika kwa miaka sita, leo unagombea Uspika wa Bunge hatuna shida na uzoefu wako. Tunataka kujua umejipangaje kuweza kuiondoa sintofahamu kwa Watanzania ya kulinda heshima na hadhi ya Bunge kuweza kujisimamia. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Karibu.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa ili niweze kujibu swali hili.

Waheshimiwa Wabunge ambao ndio wapiga kura siku ya leo na wajumbe wa mukutano huu, Mheshimiwa hapa ametaka kufahamu picha iliyoko kwa wananchi na namna ambavyo Bunge hili linafanya kazi. Mbunge ameeleza wazi kwamba ushirikiano kati ya Serikali na Bunge, ushirikiano kati ya mhimili mitatu hauna tatizo. Isipokuwa tatizo linakuja ambapo mhimili mmoja unaingilia shughuli za mhimili mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka sita kama alivyosema na mwaka huu pengine unakuwa wa saba, lakini umekuja kwa namna tofauti ambayo mimi nakuwa mgombea wa nafasi hii. Tumeifanya hiyo kazi sisi kama Bunge kwa sababu na mimi nilikuwepo kipindi ambacho mimi nilikuwa kiongozi, tumeifanya hiyo kazi kwa namna ambavyo Katiba inatuelekeza. Hakuna mazingira yoyote ambayo Serikali illiliingilia Bunge katika shughuli zake na hakukuwa na mazingira ambayo Bunge illiliingilia majukumu ya mhimili mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama nilivyooleza hapo awali mkinipa ridhaa ya kuwa Spika, Bunge hili litaendeshwa kwa mujibu wa Katiba, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni tulizojiwekea wenyewe. Kwa hivyo, Katiba na nadhani pengine nipate fursa ya kulieleza hili vizuri watu wafahamu tofauti. Bunge tumepewa kazi zetu na zile kazi zetu tulizopewa ndizo tunazopaswa kufanya. Sasa kuna mazingira ambayo

watu pengine huwa wanafikiri kwa kuwa sisi ni wawakilishi wa wananchi na kama nilivyosema sisi ni daraja kati yetu na Serikali. Watu huwa wanafikiri basi hili daraja huwa linaweza kukaa kwa namna fulani hivi ili gari isipite, ili kuzuia pikipiki isipite hapana. Kama ni daraja ni kazi yako kuhakikisha Serikali inapeleka maendeleo kwa wananchi. Wakati huo huo daraja hilo hilo liwezeshe mawazo ya wananchi, changamoto za wananchi lazima ziifiki Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila mhimili unafanya kazi zake na niwatoe hofu wananchi kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amesema, sisi humu ndani tuko vizuri na tunaelewa sawasawa na wananchi pia wanaelewa sawasawa, lakini niwatoe wasiwasi wa kufikiri pengine Bunge litaendeshwa kwa namna fulani hivi, pengine kutakuwa na unyonge hivi, hakuna unyonge mahali popote. Waheshimiwa Wabunge ambaa mmewachagua wanao uwezo wa kuisimamia Serikali, wanao uwezo wa kuishauri Serikali, wanao uwezo wa kuiwjibisha Serikali pale itakapohitajika.

Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi na kwa kuwa wananchi ndio ambaa wametuleta humu ndani, sisi kama wawakilishi wao tutaendelea kusikiliza mawazo yao ili tuyalete upande wa Serikali. Mimi nikipewa ridhaa ya kuwa Spika nitahakikisha Wabunge wanapata fursa hiyo humu Bungeni, lakini hata mazingira ya nje ya Bunge ili waweze kufanya kazi yao ya uwakilishi vizuri. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Agnes.

MWENYEKITI: Swalii la tatu.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Hapana sijakuita bado, wauliza maswali wako wengi.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Francis.

MWENYEKITI: Wengine wameandika na *message* hapa lakini Ng'enda na Francis mliandika pamoja. Sasa naomba nikupe Ng'enda, uliza swali.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa nataka niseme Mheshimiwa Mgombea tunaukiri uwezo wako katika ubobezi wa masuala ya sheria, tunaukiri uwezo wako katika kumsaidia Spika kama Naibu Spika kwa kipindi cha miaka sita tumeuona uwezo mkubwa sana. Mimi sina shaka kabisa kwamba tunapokwenda kupiga kura inawezekana ikawa historia ya kupata asilimia 100, lakini nina jambo ambalo ningependa kama swali kwako na kwetu kwamba, tumeshuhudia katika kipindi hili kutokana na sheria na kanuni tulizoziweka, shughuli zote za Bunge zinasimama kutokana na kuwepo wazi kwa kiti cha Spika. Jambo hili ni changamoto kwa sababu mhimili huu hauwezi ukawa ni wa Spika peke yake.

Je, una mpango gani ukiingia katika nafasi ya Uspika kuangalia sheria na kanuni hizi ili ziweze kurekebishwa. Shughuli za Bunge ziwe zinaendelea hata kiti cha Spika kinapokuwa wazi kwa sababu anao wasaidizi wengine? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Karibu mgombea.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Swali la Mheshimiwa Mbunge linahusu kusimama kwa shughuli za Bunge kiti cha Spika kinapokuwa wazi. Hili si jambo la kikanuni wala kisheria ni jambo la Kikatiba na kwa namna Katiba yetu ilivyo, sitaki kutoa ahadi ambazo hazitaleta ufanisi katika utendaji wa kazi. Hata hivyo, Spika ndiye anayekuwa kiongozi mkuu wa mhimili wa Bunge. Kwa hivyo, pamoja na kwamba anakuwa na wasaidizi huo mhimili kiongozi mkuu anakuwa hayupo. Ni vile vile ambavyo na safari hii tumepata huo uzoefu kwamba, upande wa Serikali na upande wa nchi. Kiongozi wa nchi

anapokuwa hayupo mazingira yametajwa kwenye Katiba nini kifanyike ili kile kiti kisibaki wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, jambo ambalo naweza kusema pengine kwa sababu sisi ndio Wabunge, siwezi kusema hapa kwamba hilo jambo tutalibadilisha, lakini pengine tunaweza kuweka utaratibu wa namna ya kumpata huyo Spika ambao unaweza ukarahisisha jambo hili kufanyika. Hata hivyo, kusema kwamba shughuli ziendelee wakati mkuu wa mhimili hayupo hilo kidogo itakuwa mtihani, nami kama mgombea sitaki kusema kwamba nikiingia mimi ndio nitabadilisha hilo. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson maswali matatu yameisha ingawa wengi wameniandikia *message*. Nisamehe sana Francis Isack, Mbunge wa Iramba Mashariki mllleta *message* pamoja. Ulikuwa na nia njema ya kuuliza swali lakini maswali matatu yameisha.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ziliuka pamoja ungetupa nafasi hivyo hivyo. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Sasa jicho la Mwenyekiti la upande huu liliona zaidi kwa hiyo, utaniwia radhi sana.

Basi tunakuruhusu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson unaweza kuendelea, maswali yameisha. Karibu sana omba kura na uweze kuendelea. (*Makofi*)

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge ambao ndio wajumbe wa kikao hiki cha uchaguzi naombeni kura zenu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa wewe unaruhusiwa kukaa kwenye kiti chako ili upige kura. (*Makofi*)

MHE. AGNES M. MARWA: Tuna imani na Tulia.....

MWENYEKITI: Hapana, hapana, hapana hairuhusiwi.

MBUNGE FULANI: Kiherehere hicho. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tumepata fursa ya kuwasikia wagombea wetu wote tisa kazi inayofuata sasa ni kupiga kura. Hivi punde tutasambaza karatasi ambazo zimeandikwa majina yote tisa na kila mmoja atatakiwa kuchagua mtu mmoja. Hata hivyo, nataka nitoe ufanuzi ambaao aliutoa mgombea namba sita Saadoun Abraham Khatib, alikuja kurekebisha jina lake hapa, lakini sisi tumeandika jina kwenye karatasi ya kupigia kura kwa jinsi tulivyolipokea kutoka Tume ya Uchaguzi. Kwa hiyo, atatuwia radhi sana karatasi yetu tutakayoigawa hapa tutaigawa karatasi inayomweleza kuwa ni Bwana Saidoun Abraham ile (i) hatujaiondoa kwenye karatasi ya kupiga kura. Kwa sababu, Tume ya Uchaguzi imetuletea jina hilo kama liliuyoandikwa. Kwa hiyo, asije akashangaa akakuta jina lake liko namna hilo.

Wabunge waliopo leo humu ndani ni 372, kwa hiyo, tutapiga kura Wabunge 372. Nafurahi kumuona na Jerry Silaa leo amekuja nadhani na Mheshimiwa Gwajima wamekuja leo. Kwa hiyo, baada ya kazi hii ya kujieleza kukamilika kama ilivyo ada ndugu zangu, tuna uzoefu wa kupiga kura sana nisiongeze maneno mengi. Niwaruhusu sasa wale wanaogawa karatasi za kura wagawe ili kila mmoja aweze kutumia haki yake ya kikatiba. Katibu gaweni karatasi kila mtu achukue karatasi moja. (*Makofi*)

(Hapa karatasi za kupigia kura ziligawiwa kwa Wabunge)

MWENYEKITI: Majina yako tisa, wamejieleza wote chagua jina moja unayefikiri anafaa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tafadhali msome vizuri hiyo karatasi mtiririko ulivyoandikwa ni tofauti na walivyojieleza kwa hiyo someni vizuri.

Ili boksi liweze kutumbukiza vizuri kunjeni mara nne hivi ili muweze kutumbukiza vizuri.

Jamani kule karatasi bado, huku bado, wagawa karatasi wako wapi? Mama changamka, Chima yuko wapi? Changamka kugawa karatasi kule.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, boksi namba moja liko wapi? Tunataka tuweke karatasi.

MWENYEKITI: Mama changamka hapo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mjambe mbona una moto hivyo? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Ngoja tumalize kupiga halafu tutakuja kukusanya. Wote mmepata karatasi?

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado.

MWENYEKITI: Jamani vipi?

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado.

MWENYEKITI: Harakisheni basi, hawa wagawa karatasi leo *ma-learner* nini? Hebu wanyooshe mikono ambao hawajapata karatasi *please*. Mnaona wagawa karatasi vipi? Kila mtu achukue karatasi moja tu, haya gaweni huko. Haya mikono hiyo huko bado hapo, wale ambao hawajapata karatasi upande huu wanyooshe mikono. Haya kila mtu ahakikishe amepata karatasi huku tayari wametimia. Upande huu? Haya bado pale akina Shabiby bado hawajapata, hebu angalia hapo kwa Mheshimiwa Shabiby bado hajapata. Tutulie kidogo.

Haya nadhani wote mmeshapata sasa. Wote mmepata karatasi?

WABUNGE FULANI: Ndio.

MWENYEKITI: Mmeshapiga kura?

WABUNGE FULANI: Ndio.

MWENYEKITI: Haya Chima anza kukusanya kura, kusanyeni kura.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, waombe kila mstari wakusanye.

MWENYEKITI: Mnaweza mkakusanya ili watu wapite barabarani huko. Pelekeni hiso karatasi kwenye kona ili wale wapiti barabarani. Haya, wakusanyaji piteni mkusanye. Kusanyeni kwenye kona huko wanakopita, pelekeni huko barabarani. Haya, chukua na ya Mwenyekiti hapa, usimsahau eh!

Jamani, mmemaliza wote? Ambao kura zao bado wanazo mkononi wanyooshe mkono.

MBUNGE FULANI: Tumemaliza.

MWENYEKITI: Kura zote ziwekwe kwenye maboksi. Jamani, wote tumepeiga kura?

WABUNGE FULANI: Ndiyo!

MWENYEKITI: Tumetumbukiza kwenye maboksi?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MWENYEKITI: Kama kuna mtu hajaweka kura kwenye boksi, hatutafungua tena hilo boksi. Narudia mara ya mwisho, wote tumeweka kura kwenye boksi hiso?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MWENYEKITI: Haya. Kwa hiyo, kazi ya kupiga kura imekamilika. Ninyi sogeeni huku kidogo, niwaite wengine hapo.

Haya, kwa kuwa sasa kazi ya kupiga kura imeisha, tunaweka lakiri kidogo.

Sasa kwa ruhusa yenu, kwa kuwa kazi ya kupiga kura imeisha, kwa utamaduni wetu huwa tunawauliza wagombea kama wana mtu ambaye wangependa aende akawasimamie kwenye kura zao. Sasa akina Chima ondokeni kidogo tuwapishe wakubwa zenu wanakuja.

Ndugu zangu, sasa nafikiri wale wagombea tuwape fursa, kama wanataka kutoa mwakilishi mionganini mwetu aende akawasimamie. Ninaanza na mtu wa mwisho kwenye orodha yangu ya kujieleza.

Hallow, watasimama pale, hayo masanduku yawekeni hapa.

MWENYEKITI: Mgombea, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson unayo fursa ya kutoa mwakilishi kama ungependa aende akakusimamie kura zako, lakin pia unayo fursa ya kusema unaiamini Meza; yote mawili unaweza kusema.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiamini Meza kwa maana ya Mwenyekiti na Wasaidizi wako. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Haya. Naomba kwa ruhusa yenu Waheshimiwa Wabunge niwaite Wagombea wengine.

MBUNGE FULANI: Waomba ridhaa.

MWENYEKITI: Waomba Ridhaa nimeambiwa. Waingie hapa.

(Hapa Wagombea nafasi ya Kiti cha Spika wengine waliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Naomba mje hapa tafadhali, msimame hapa mstari halafu nitawapa maelezo. Mnaweza mkajipanga hivi, halafu mkawaangalia wapiga kura. Waangalieni Wapiga kura.

Waheshimiwa Wagombea, kwa utamaduni tu tuliouzoea, mgombea anaweza akaleta mwakilishi wa kumhesabia kura au anaweza akaiamini Meza vile anavyoona. Kwa hiyo, naomba nimwulize mmoja mmoja.

Bwana Abdullah Mohamed Said, kuna mtu unataka aingie au unalamini Meza?

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Mke wangu.

MWENYEKITI: Mke wako yupo juu. Hapana, hawezি kutoka mtu wa juu, ni humu ndani. Wewe ndiye tumekuombea kibali uingie humu ndani.

NDG. ABDULLAH MOHAMED SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hiyo. Watu nilionao wako kule juu, lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge wangu wa Jimbo la Ziwani asimamie kura zangu. (*Kicheko/Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngwali.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. DEO K. SANGA: Kama inawezekana wanaweza kwenda hata wao wenyewe. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ngoja waseme wenyewe. Wana uwezo wa kuwaita hata Wabunge, siyo lazima waende wao. Haya, Mheshimiwa Ngwali utasimama hapo. Sasa Mheshimiwa Abdullah Mohamed Said unaweza kwenda nje, mwakilishi wako yupo. Nenda nje tu.

(Hapa Nd. Abdullah Mohamed Said Aliondoka Ukumbini)

MWENYEKITI: *Engineer Aivan Jackson Maganza* unapenda nani akuwakilishe katika jambo hili? Chagua yeoyote unayemtaka.

ENG. AIVAN JACKSON MAGANZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa naona mchakato unaenda kidemokrasia, nami ningeomba niiamini Meza. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nenda Bwana Ivan.

(*Hapa Eng. Aivan Jackson Maganza Aliondoka Ukumbini*)

MWENYEKITI: Mgombea wa tatu ni Ndugu David Daud Mwaijojele, kama unaona Mwenyekiti wako anakutosha, mimi nipo kukuwakilisha.

NDG. DAVID DAUD MWAIJOJELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mke wangu ni wa Iringa, najua Mwenyekiti utanisimamia vema. Nimewomba Mwenyezi Mungu, amewagusa wote watanipa kura. (*Kicheko/Makofi*)

Ahsanteni sana. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(*Hapa Ndg. David Daud Mwaijojele Aliondoka Ukumbini*)

MWENYEKITI: Pia namwomba Ndugu Georges Gabriel Bussungu. Maelezo ni hayo hayo.

NDG. GEORGES GABRIEL BUSSUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, niniamini Meza, haina shida. (*Makofi*)

(*Hapa Ndg. Georges Gabriel Bussungu Aliondoka Ukumbini*)

MWENYEKITI: Namba tano ni Ndugu Kunje Ngombale Mwiru.

NDG. KUNJE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tumejawa na uzalendo, amani, utulivu, demokrasia safi na salama. Nchi yetu ni mfano wa kuigwa duniani kote kwa ujumla. Kwa hiyo, ninaamini meza hizo walizokaa Waheshimiwa Wabunge, ni Watanzania wenzangu na wana imani nami, nami ninawaamini. Basi ninawashukuru kwa kitakachopatikana.

Ahsanteni sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante.

(*Hapa Nd. Kunje Ngombale Mwiru Aliondoka Ukumbini*)

MWENYEKITI: Ndugu Maimuna Said Kassim.

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Naomba Mheshimiwa Ummy Mwalimu anisimamie kura zangu. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Ummy Mwalimu atafutwe. Ahsante sana. Tutamtafuta Mheshimiwa Ummy Mwalimu unaweza kwenda. (*Kicheko*)

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Hayupo!

MWENYEKITI: Atakuja tu. Mtafuneti Mheshimiwa Ummy Mwalimu amependekezwa hapa. Atafutwe Mheshimiwa Ummy Mwalimu amwakilishe Mheshimiwa Maimuna. Mwiteni Mheshimiwa Ummy Mwalimu huku.

Chief- Whip mwite Ummy Mwalimu aje afanye kazi hapa. Mpigie simu popote alipo, ana kazi kubwa hapa. (*Kicheko*)

(*Hapa Nd. Maimuna Said Kassim Aliondoka Ukumbini*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Bwana Ndonge Said Ndonge, karibu. Ulinifurahisha sana.

NDG. NDONGE SAIDI NDONGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi bwana nina Wakala wangu anaitwa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo. Wakala, matokeo uniletee na usiponiletea hapa, utaniletea Jimboni. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Haya karibu sana Mheshimiwa Chaurembo.

(Hapa Ndg. Ndunge Saidi Ndunge Aliondoka Ukumbini)

MWENYEKITI: Bwana Saadun, kwanza nikuombe radhi sana. Bila shaka ulinisikia au hukunisikia. Ulisahihisha jina lako tuondoe 'i', tumeshindwa kuiondoa. Kwa hiyo, karatasi yetu ya kupiga kura imeenda na jina hilo lenye 'i' kwa sababu Tume ya Uchaguzi walituletea jina lako likiwa na 'i'. Tuwie radhi sana. Kwa hiyo, hapa sisi tutakutambua kwa jina hilli, lakini kwa sababu umerekebisha, mimi nitakutamka wewe ni Saadun Abdulrahman Khatib. Karibu utuambie na wewe.

NDG. SAIDOUN ABDULRAHMANI KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mashaka yoyote na utendaji na mchakato mzima wa shughuli hii, kwa sababu uzalendo kwanza na mambo mengine baadaye. Ningependa kumweka Wakala wangu Mheshimiwa Selemani Jafo anisimamie. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Selemani Jafo. Mheshimiwa Ummy amepatikana? Eeh, unasemaje Naibu Waziri.

(Hapa Ndg. Saidoun Abdulrahmani Khatibu Aliondoka Ukumbini)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ummy ameomba Mheshimiwa Ulenge amsaidie.

MWENYEKITI: Hapana, basi tumwite yule mama ataje mtu mwininge.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Sawa.

MWENYEKITI: Mwite Ndugu Maimuna Said Kassim aje tena.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Naomba tafadhali aje Bi. Maimuna tumpe fursa ya pili. Labda kwa sababu alimpenda Waziri wa Afya, anaweza akamteua Naibu.

(Hapa Ndg. Maimuna Said Kassim Aliingia Ukumbini)

MWENYEKITI: Bi. Maimuna tunaomba radhi kidogo, uliyempenda sana ameomba udhuru hapa kwa *Chief-Whip*, yupo nje kikazi, lakini kura yako ameshakupa bila shaka. (*Kicheko*)

Sasa tunao wengi hapa bila shaka, kama unaiamini Meza sema, na kama unatafuta mtu mwingine, wapo hapa.

NDG. MAIMUNA SAID KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nimchague kaka yangu, Mheshimiwa Omari Kigua. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Unaona hayo! Haya, Mheshimiwa wa Kilindi, mgombea mwenzake huyo.

(Hapa Ndg. Maimuna Said Kassim Aliondoka Ukumbini)

MBUNGE FULANI: Na suti zao zinafanana.

MWENYEKITI: Ni mgombea mwenzake na alipata kura 18,000 ametuambia hapa, siyo! Karibu sana.

Hawa ni Wawakilishi maalum. Nami namteua Mwakilishi wa Mwenyekiti maana Mwenyekiti hawezu kuingia huko. Mheshimiwa Almas upo?

WABUNGE FULANI: Yupo.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Almas njoo, wewe ni Mwakilishi wa Mwenyekiti, utaingia huko. Wewe unaniwakilisha mimi na hawa wanawakilisha waliowataja. Haya ingieni ndani. Akina Chima ingizeni ndani hayo maboksi. (*Makofî*)

Tafadhalii Waheshimiwa, ninyi mmekwenda kwa *interest* za wale waliowatuma kusimamia kura za kila mgombea wako. Utakayoyakuta huko ni ya kwako mwenyewe. Mheshimiwa Almas, wewe ni jicho langu huko ndani, sawa!

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Ndiyo.

MWENYEKITI: Eeh! Wewe utahakikisha yanayokuja kwangu ndiyo yale yametimia. Nanyi mtashuhudia kwa macho yenu ili muwe mashahidi wa Wagombea na Bunge hili kwamba matokeo yatakayokuja kwangu mmeshuhudia na mmeyaona vizuri. Tumeelewana vizuri?

WAWAKILISHI WA WAGOMBEA: Ndiyo.

MWENYEKITI: Basi aanze kuingia Mwenyekiti kwanza. Tangulia.

Mheshimiwa Jafo, umemsahau mgombea wako? (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapa, nasitisha kikao kidogo kwa muda wa dakika 20 mpaka saa sita na nusu.

Ahsanteni sana. Hakuna Siwa, ni utawala binafasi.

(*Saa 5.55 Kikao killisitishwa hadi Saa 6.30 Mchana kupisha zoezi la kuhesabu kura*)

(*Saa 6.30 Mchana Bunge lilitrudia*)

MWENYEKITI. Haya Katibu gonga kengele hapo. Gongeni kengele watu waingie. Haya Waheshimiwa Wabunge tukae. Ee bwana, umepiga kengele kule? Mbona watu hawaingii!

Waheshimiwa naomba tukae tumalizie kazi na wale Waheshimiwa waliopo nje waingie.

Waheshimiwa Wabunge, kazi iliyotuweka hapa tangu saa tatu inafika ukingoni. Mbele yangu hapa ninayo karatasi ya matokeo ya kura mlizopiga na zimethibitishwa na wawakilishi wa wagombea wote pamoja na mwakilishi wa Mwenyekiti. (*Makof*)

Kwa hiyo kwa heshima na taadhima naomba nitangaze matokeo kama ifuatavyo:-

Tulipoanza nilisema wapiga kura walikuwa 372, lakini baadaye waliongezeka wanne. Kwa hiyo mliopiga kura leo mlikuwa 376. Waheshimiwa Wabunge mliopiga kura leo ni 376.

MATOKEO YA UCHAGUZI

MWENYEKITI: Sasa naomba mniruhusu, nasoma matokeo kwa kadri ya karatasi niliyoitumia wakati wa kuwaita kujieleza. Narudia tena, matokeo haya yamethibitishwa na Mheshimiwa Jafo kwa mgombea wake, Mheshimiwa Mbunge wa Kilindi umethibitisha kwa mgombea wako, Mheshimiwa Ngwali bila shaka umetia na saini hapa, Mheshimiwa Chaurembo nawe umethibitisha alichopata mpiga kura wako na mwenyekiti wangu pale amethibitisha yaliyopatikana na sahihi ninazo.

Wa kwanza niseme Bwana Abdullah Mohamed Saidi, hakupata kura hata moja. (*Makof*)

Mgombea wa pili alikuwa *Engineer Ivan Jackson Maganza*, naye kura hazikutosha, hakupata hata moja. (*Makof*)

Wa tatu, Ndugu David Daud Mwaijojele, hakupata kura hata moja. (*Makofi*)

Wa nne, Bwana Georges Gabriel Bussungu, huyu naye hakupata kura hata moja. (*Makofi*)

Wa tano, Bwana Kunje Ngombale-Mwiru, hakupata kura hata moja. (*Makofi*)

Wa sita, Bi Maimuna Saidi Kassim, hakupata kura hata moja. (*Makofi*)

Wa saba, Bwana Ndonge Saidi Ndonge, yule aliyeupiga mwingi na aliyesema ukweli kuwa Mama Samia kaupiga mwingi, lakini hapa, mmh! Hakupata kura. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, yale aliyojasema ni kweli, Mama Samia kaupiga mwingi, yale ni ya kweli na tuzo nyingi amepewa pale, najua amepata tuzo za kutosha kwa maneno ya ukweli aliyojasema, lakini muda haujafika. Wajumbe hawa hawatabiriki hawa, akina Esther hawa, wanamchekea halafu wanamnyima kura. (*Makofi/Kicheko*)

Haya, wa nane ni Bwana Sadun Abdulrahman Khatib, huyu mwakilishi wake alikuwa Mheshimiwa Ngwali, hakupata kura. (*Makofi*)

Wa tisa ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, huyu ni mgombea wa Chama Cha Mapinduzi, amepata kura zote 376. (*Makofi/Vigegele*)

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba Wimbo wa
"tuna imani na Tulia")*

MWENYEKITI: Kwanza, niwapongeze sana. Hili ni Bunge la Karne ya 21 kweli, hakuna kura iliyoharibika. Kwa hiyo, kwa mamlaka niliyo nayo, mliyonipatia ninyi, nataka nimitangaze mliyemchagua leo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson.
(*Makofi/Vigelegele*)

Naomba Wabunge wachache wamtafute huko aliko ili aje asikie matokeo yake hapa, aletwe hapa, mleteni hapa Dkt. Tulia Ackson. Mheshimiwa Esther na wewe nakuteua kamtafute Dkt. Tulia. Mheshimiwa Lucy pia kamtafute Mheshimiwa Spika. (*Makofi*).

*(Hapa Mhe. Dkt. Tulia Ackson Aliingia Ukumbini
Akisindikizwa Wabunge Wakiimba)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Nimkaribishe Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KIAPO CHA SPIKA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hatua inayofuata ni Kiapo cha Spika, lakini nitoe maelezo kidogo, subiri kidogo. Baada ya kiapo hiki mimi nitamsindikiza Mheshimiwa Spika, maana tayari Mheshimiwa Spika atakuwa nje, halafu atarudi rasmi akiwa Spika, sisi tukiwa tumetulla hapa. (*Makofi*)

Naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi hii mliyonipa, Mungu awabariki sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu tumeendesha kwa heri. Nirudie yale yote ambayo tunesema, tunaamini Bunge letu ni moja na tunaamini kwamba Spika tuliyemcagua huyu atakuwa ni mlinzi na mlezi wa mhimili huu wa Bunge. (*Makofi*)

Kama tunavyomjua, Mheshimiwa Dkt. Tulia anajua kwamba pamoa na kwamba ye ye ni Kiongozi wa Mhimili lakini kuna kiongozi wa nchi. Kuna Mkuu wa Nchi na kuna Amiri Jeshi Mkuu, anajua mipaka yote hii, kwamba ye ye ni mhimili wa Bunge, lakini yuko Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anaitwa Samia Suluhu Hassan, hilo analijua.

Kwa hiyo, baada ya hapo, nitashuka, tutakwenda kusikiliza kiapo, halafu baada ya hapo nitamsindikiza Mheshimiwa Spika, lakini sisi tutulie humu ndani ili baadaye Mheshimiwa Spika aje kumalizia mambo yake. Nami kwa hapa cheo changu kimefutwa. (*Makofii*)

Mhe. Dkt. Tulia Ackson

*(Hapa Spika wa Bunge Mhe. Dkt. Tulia Aliapa
Kiapo cha Spika)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. William V. Lukuvi) Alikamilisha
Kazi yake*

Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa tukae. (*Makofii*)

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE

KIAPO CHA UAMINIFU

Mbunge afuataye aliapa:-

Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai

SPIKA: Katibu!

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninayo taarifa hapa kutoka Ofisi yangu.

Katika Mkutano wa Tano wa Bunge, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 6) ya Mwaka 2021 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 6) Bill 2021*).

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hiyo, napenda kulitaarifu Bunge hili tukufu kuwa tayari Muswada huo umepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria ya nchi inayoitwa, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) Sheria (Na.10) ya Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6) Act. (No.10) of 2021*].

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ameshaweka sahini kweneye Muswada huu na kwa hiyo, umekuwa sheria na hivyo imepitishwa rasmi. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, katika Orodha ya Shughuli tulizokuanazo Mezani tumekamilisha na sasa naomba nichukue fursa hii kusema machache, halafu nitaleta matangazo ya wageni tulionao hapa ndani na pia matangazo ya shughuli ambazo ni za Bunge kwa utaratibu wetu tuliojiwekea. (*Makofii*)

SHUKURANI ZA SPIKA

SPIKA: Kwanza kabisa nianze kumshukuru sana Mwenyekiti wetu ambaye amesimamia Uchaguzi huu kwa mujibu wa kanuni zetu, kanuni namba 9(5) inayozungumza kuhusu Uchaguzi wa Spika. Kwa hiyo, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi tunakushukuru sana Wabunge wote na mimi pia kwa kazi nzuri uliyoifanya siku ya leo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumshukuru Mwenyekiti kwa niaba yenu nyote, lakini kwa niaba yangu mwenyewe, pia nichukue fursa hii kumshukuru sana sana Mwenyezi Mungu ambaye ametupa fursa sisi wote wa kuwa hapa siku ya leo kushuhudia jambo hili na kufanya jambo hili kubwa liliofanyika mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi, uchaguzi wa Spika siyo jambo dogo, ni jambo kubwa. Ni jambo la kikatiba na jambo la kisheria. Leo tumelikamilisha vizuri kwa utulivu na kwa mshikamano wa hali ya juu sana. Mshikamano huu ninyi nyote ni mashahidi kwamba heshima mliyonipa mimi

niliyesimama mbele yenu hapa, mmenipa kura zote za Wabunge wote waliohuduria siku ya leo. Ninawashukuru sana sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa ni muda muafaka wa kutoa neno la shukurani kwenu na wote ambao wamefanikisha mchakato huu. Nimemshukuru Mheshimiwa Lukuvi, lakini shukrani za kipekee zikiendee Chama cha Mapinduzi, kwa sababu mara baada ya tarehe ya kuchukua fomu kutangazwa tulijitokeza Wana-CCM 71 kuhitikia wito huo. Chama chetu kilitoa nafasi kwa wanachama wake wa jinsia zote wenye uwezo, ujuzi na uzoefu wa aina mbalimbali walijitokeza. Tulifanya hivyo kwa uhuru mpana na kwa nafasi sawa. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, ukomavu huu wa kidemokrasia ni wa kupigwiwa mfano. Ninakishukuru sana Chama chetu kwa kutoa fursa hiyo ambayo iliniwezesha mimi kuwa mmoja ya wale walijitokeza kugombea nafasi hiyo. (*Makof!*)

Mnamo tarehe 20 Januari, 2022 Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi ilikaa hapa Jijini Dodoma kupitia na kuchambua orodha ya Wana-CCM walijitokeza chini ya uongozi mahiri ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Samia Sululu Hassan. Kamati kuu kwa kauli moja iliteua jina la Tulla Ackson kupeperusha bendera ya CCM katika kinyanganyiro cha kumpata Spika. (*Makof!*)

Kwa mnasaba huu na kwa namna ya kipekee, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa Wajumbe wote wa Kamati Kuu kwa uteuzi huo walioufanya. Kama inavyofahamika, kanuni zetu zinaruhusu Spika kutoka nje au ndani ya Bunge kuteua jina moja la mgombea ambaye pia ni Mbunge, ni ishara muhimu kwangu binafsi lakini kwa Mbunge letu. Ni imani ya Chama cha Mapinduzi kwetu sisi Wabunge. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama chama kiliona vyema kufanya hivyo, naamini sisi wote tunakubaliana na imani hiyo wallyoionesa na bila shaka kura mlizozitoa siku ya leo Wabunge wenzangu wote mmekubaliana na imani hiyo ya Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, leo hii mimi Mbunge mwenzenu nisingefika hatua hii ya kusimama mbele yenu kama Spika kama siyo wingi wa kura zenu. Naomba mpokee shukurani zangu za dhati kwa kunipa kura za kishindo zilizoniwezesha kupata heshima hii kubwa ya kuwa Spika. Imani kubwa mlionionyesha itakuwa chachu ya utendaji wangu katika kulitumikia na kuliongoza Bunge letu. Kama tulivyoshikamana leo, basi tuendelee kushikamana katika kuwatumikia wananchi wenzetu na kusimamia maslahi ya Taifa letu.

Waheshimiwa Wabunge, upo usemi maarufu usemao, "*In Africa it takes a village to raise a child.*" Kwa tafsiri nyepesi, ni Barani Afrika yataka Kijiji kukuza mtoto. Usemi huu una ukweli kwa wengi wetu ambaa tumezaliwa na kukulia vijijini.

Mimi nilizaliwa na kukulia katika Kijiji cha Buliaga. Nililelewa na wazazi wangu; mzee wangu, baba yangu mzazi, Ackson Mwansasu ambaye alitangulia mbele za haki, lakini na mama ambaye siku ya leo yuko hapa, anaitwa Nkundwe Nsasu. (*Makofi*)

Nilikuzwa na shangazi, wajomba, bibi, babu; nilikuzwa na Kijiji. Leo hii ninayo furaha kumtambulisha kwenu Mwakilishi wa Kijiji hicho kilichonikuza, mama yangu mzazi, Bibi Nkundwe Nsasu ambaye yuko hapa. Pengine asimame ili muweze kumfahamu. (*Makofi/Vigelegele*)

*(Hapa Mama Mzazi wa Spika, Bibi Nkundwe Nsasu
Alisimama akiwa Gallery ya Spika)*

SPIKA: Ahsanteni sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Kupitia kwake tunaendelea kutoa shukurani za malezi hayo na makuzi bora. Kwa hiyo, Kijiji kizima kilichohusika katika maisha hadi kufikia hapa, ye ye ametuwakilisha. Ninawashukuru sana wote. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, ni wazi kwamba katika safari iliyonifikisha hapa leo nimekuzwa pia na vijiji vingine vingi, siwezi kuvitaja vyote itoshe tu kusema kwamba toka nilipoanza Shule ya Msingi hadi kuhitimu elimu ya Chuo Kikuu, nimelelewa na kukuzwa na wengi. Ninawashukuru kwa dhati Walimu wangu, viongozi wangu na wote ambao wamechangia safari ambayo leo imenifikisha katika nafasi ya juu kabisa ya Uongozi wa Bunge letu. (*Makof*)

Katika Kijiji hiki cha Bunge nilipo hivi sasa, nimepata vile vile malezi mazuri na makuzi mema. Ninyi nyote Waheshimiwa Wabunge mmenilea na kunikuza. Napenda nichukue nafasi hii nimirage na kumshukuru sana Spika Mstaifu, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Ndugai alinifunza mengi, alinielekeza, alinishauri na aliniongoza vizuri kama Mbunge na kama msaidizi wake katika uendeshaji wa Bunge letu. Alinipa fursa mbalimbali ambazo zililenga kuboresha utendaji kazi wangu katika kipindi chote cha miaka sita niliohudumu katika nafasi ya Naibu Spika. Tunamshukuru na kumtakia maisha mema ya ustaifu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kama sote tunavyofahamu, kuingia katika jengo hili sharti mtu awe Mbunge. Naendelea kumshukuru Rais wa Awamu ya Tano, Marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.... (*Makof/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. (*Makof*)

....ambaye alinitua kuingia katika Bunge hili kwa mara ya kwanza mwezi Novemba, 2015. Tunamwomba

Mwenyezi Mungu aendelee kumpumzisha kwa amani.
(Makofii)

WABUNGE FULANI: Amen.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mwaka 2020 nilijitosa kugombea Ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi kufuatia uchaguzi uliofanyika tarehe 28 mwezi wa 10, 2020 na niliibuka mshindi wa kiti hicho. Ni dhahiri kwamba nisingeweza kupata nafasi nyingine ya kuingia Bungeni pasipo kura za wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini.

Ninawashukuru sana wapiga kura wenzangu kwa kuniamini na kunipa kura nyingi zilizoniwezesha kuwa Mbunge. Hivi leo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameona ninafaa kuhudumu katika nafasi hii ya Spika. Ahsanteni sana Wana-Mbeya Jiji. *(Makofii)*

Kwa nafasi hii pia napenda kuwashukuru pia wagombea wenzangu ambao wote tumepata fursa ya kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu siku ya leo. Yote hii ni kutokana na kwamba hao ambao wamejitokeza wametumia nafasi yao ambayo Katiba inawaruhusu kufanya hivyo. Ni imani yangu kwamba baada ya Spika mpya kupatikana tutaungana sote kwenye safari yetu ya pamoja ya kuwatumikia wananchi na kujenga nchi yetu iwe imara kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kwa pamoja tuijenge Tanzania yenye umoja na mshikamano chini ya uongozi madhubuti wa Rais wetu Mheshimiwa Suluhu Hassan akisaidiwa na viongozi wetu wakuu wa pande zote mbili za Muungano. *(Makofii)*

Waheshimiwa Wabunge, nilisema katika utangulizi kwamba salamu zangu hizi ni za shukrani. Hivyo, naomba kwa mara nyingine wote niliowataja ama mmoja mmoja au kwa makundi wakubali shukrani zangu hizi za dhati. *(Makofii)*

Naomba sasa mniruhusu nizungumze kidogo kuhusu kazi kubwa iliyo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tunapoipanga kutekeleza majukumu yetu kama Wabunge, mimi binafsi kama Spika wa Bunge letu Tukufu, hatuna budi kujikumbusha baadhi ya dira kuu zitakazoongoza kazi inayotusubiri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mojawapo ya dira kuu hizo ni hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliyoitoa Bungeni mnamo tarehe 22 Aprili, 2021. Katika hotuba hiyo, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliainisha vipaumbele kadhaa vyta Serikali ya Awamu ya Sita. Baadhi ya hivyo alivitaja kuwa ni: kwanza, kuimarisha uchumi wa nchi, kupitia kukuza biashara, kuvutia wawekezaji, kuongeza makusanyo ya kodi na kukuza uchumi kwa 8%. (*Makofii*)

Pili, kuimarisha uchumi wa wananchi ikiwemo kupunguza ukali wa maisha, kudhibiti mfumuko wa bei, kuongeza kipato na ajira, kuondoa kero katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Tatu, kuimarisha huduma na ustawi wa jamii kama vile afya, elimu, maji na kurekebisha miundombinu ya barabara, madaraja, umeme, vivuko, ikiwemo kuendeleza na kukamilisha miradi yote ya kimkakati.

Nne, kuleta nidhamu katika kusimamia rasilimali za Taifa letu na kuwawajibisha wazembe, wabadhirifu na wala rushwa wote bila kuwaonea aibu wala huruma. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hotuba ile, matumaini ya Mheshimiwa Rais ni kwamba Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watavisimamia vipaumbele hivyo na kuvitekeleza kwa umahiri mkubwa. (*Makofii*)

Kwa upande wetu sisi Wabunge, kazi yetu imeainishwa vizuri ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara 63. Kwa mujibu wa Ibara hii, Bunge

hili ndicho chombo kikuu chenye madaraka na wajibu kwa niaba ya wananchi wa kuisimamia na kuishauri Serikali, Taasisi na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, katika muktadha wa vipaumbele vyta Serikali Awamu ya Sita vilivyoainishwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Bunge hili Tukufu ni mfano wa daraja. Kwa dhamana hii mliyonipa, nitatumia nguvu zangu zote kadri nitakavyojaliwa na Mwenyezi Mungu kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa umakini ili liwe daraja madhubuti kati ya wananchi na Serikali yao. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nitaliongoza Bunge hili kuisimamia na kuishauri Serikali ili liweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Tutauliza maswali, tutaihoji Serikali kwa hekima na busara na kwa kuzingatia kiapo chetu kama Wabunge. Tutafanya hivyo kwa nia thabiti ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maendeleo wanayoyatamani na nchi yetu inapiga hatua zaidi katika nyanja zote.

Waheshimiwa Wabunge, hii ni hotuba ya shukrani. Sikukusudia nichukue muda wenu mwinci. Sasa naomba nimalizie; nimewataja wengi na nimewashukuru wengi, wote walistahili sana.

Shukrani za mwisho, lakini siyo kwa umuhimu ni kwa familia yangu, ikiongozwa na mume wangu, James Andilile Mwainyekule. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Amekuwa mzazi mahiri kwa watoto wakati wote ambao mimi nakuwa nikitimiza majukumu haya mliyonipa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, namalizia kwa kuwashukuru sana na kusema kazi iendelee. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nilete kwenu matangazo ya wageni tuliyonayo hapa na matangazo ya kazi. Tutaanza na matangazo yanayohusu wageni:-

Kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika na tutaanza na Viongozi wa Kitaifa; tunaye Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Karibu sana Mheshimiwa Spika. (*Makofii*)

Tunaye pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu. Karibu sana kiongozi wetu. (*Makofii*)

Tunaye pia Mheshimiwa Pius Msekwa ambaye ni Spika Mstaafu. Karibu sana baba yetu. (*Makofii*)

Tunaye pia Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ambaye ni Spika Mstaafu. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Mheshimiwa Balozi Hussein Katanga, Katibu Mkuu Kiongozi. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunao na wengine ambaao pia wako kwenye Jukwaa la Spika; tunaye Ndugu Boaz Ackson, huyu ni kaka mkubwa wa Spika. Ahsante sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Ndugu Adeline Ackson, huyu ni dada mkubwa wa Spika. Ahsante sana. (*Makofii*)

Tunao pia Viongozi wa Kitaifa wa Chama Cha Mapinduzi, tunaanza na Dkt. Abdullah Sadala ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Zanzibar. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia Wakuu wa Vyombo vyta Ulinzi na Usalama ambaao wameungana nasi leo; tunaye Jenerali Venance Mabeyo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Ahsante sana. (*Makofii*)

Tunaye IGP Simon Sirro, Mkuu wa Jeshi la Polisi. Ahsante sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Ndugu Diwani Athumani Msuya, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa; Ahsante sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Meja Jenerali Suleiman Mzee, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Dkt. Anna Makakala ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Uhamiaji. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Ndugu John Masunga ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye pia *CP. Salum Hamduni* ambaye ni Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Ndugu Gerald Kusanya Musabila ambaye ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevyta. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Brigedia Jenerali Andrew Chakira ambaye ni Mrakibu Mkuu Baraza la Usalama wa Taifa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Luteni Jenerali Mathew Edward Mkingule, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Brigedia Jenerali Rajabu Mabele, Mkuu wa JKT. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Anthony Mtaka ambaye ameambatana na Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini; Mstahiki Meya. Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini. Karibuni sana. (*Makofi*)

Nimeletewa tangazo hapa lakini sijaona majina yao, nimeambiwa wapo Ma-DC na Wenyeviti wa Halmashauri na Viongozi wa CCM na wengine. Sasa mtaniwia radhi, nitawataja wale ambao nawafahamu katika orodha hii; yupo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, *Comrade Juma Homera*. Karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ameongozana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dkt. Angelina Lutambi. Karibu sana. (*Makof*)

Ngoja nione kama hawa wengine wako sehemu nyingine, sawa, naona wengine wako mbele huku; karibuni sana.

Pia tunao Viongozi wa Dini ambao wamekuja leo kuungana nasi. Kwanza tunaye Dkt. Barnabas Mtokambali, Askofu Mkuu wa Kanisa la *Tanzania Assemblies of God* akiambatana na mkewe. Karibu sana Baba Askofu. (*Makof*)

Tunaye pia Askofu Dkt. Frederick Shoo, Mkuu wa KKKT na Mwenyekiti wa Baraza la Kikristo Tanzania. Ahsante sana. Baba Askofu, Dkt. Frederick Shoo ameambatana na mama. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunaye pia Dkt. Israel Mwakyolile, huyu ni Askofu Mstaafu wa KKKT, Dayosisi ya Konde. Ahsante sana na karibu sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Ndugu Jacob Mwakasole ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya. Karibu sana. (*Makof*)

Sasa hapa kwa majina, ni kwa vile nawafahamu lakini Mwenyekiti ilikuwa awakilishe uongozi wote wa CCM Mkoa wa Mbeya, lakini Mwenyekiti ameongozana na Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, pia ameongozana pia na Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi wa Mkoa wa Mbeya. Karibuni sana. (*Makof*)

Wapo na viongozi wengine ambao ameongozana nao Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa, tunawashukuru sana kwa kuja; ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa hapa taarifa kwamba Mama Kastiko ambaye ni Naibu Katibu Mkuu naambiwa yuko hapa. Samahani mama jina halikuwa

limekwa hapa nikajua umeomba radhi, simama kidogo tukuone vizuri; Mama Maureen Kastiko, Kiongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Makao Makuu, karibu sana. (*Makof!*)

Tunao pia Machifu wa Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Chifu Rocket Mwashinga; karibu sana. Yule aliyesimama naye pia ni chifu anaitwa Chifu Lyoto. Karibuni sana. (*Makof!*)

Wapo pia Viongozi wa Dini kutoka Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Kadhi wa Mkoa Sheikh Hassan Mbarazi; karibu sana. (*Makof!*)

Tunao pia Wakuu wa Wilaya ambao wako hapa lakini sijaletewa orodha ukiacha Mkuu wa Wilaya ya Dodoma hapa na wengine wote waliopo tunawashukuru sana kwa kuja; karibuni sana.

Pia yupo Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya na Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya waliopo, msimame wote kwa pamoa. Karibuni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, Mstahiki Meya ameongozana na Madiwani wote wa Jiji la Mbeya, sijui wamekaa upande gani; karibuni sana Madiwani wenzangu, ahsanteni sana kwa kuja. (*Makof!/Vigelegele*)

Vile vile najua wapo Madiwani wengine ambao wanatoka sehemu nyingine, kama wapo na wao wasimame; karibu sana. (*Makof!*)

Tunao viongozi waandamizi wa CCM wa mikoa mbalimbali lakini pia na wa wilaya waliopo, taarifa nilizonazo na wale ninaowafahamu ni wale wa Mbeya Mjini, Mwenyekiti na Katibu, sijui watakuwa wamekaa upande gani. Mwenyekiti wa Wilaya wa CCM; karibu sana Ndugu Humphrey Msomba; Katibu, Ndugu Denis Luhende, karibuni sana na viongozi wote ambao mmeongozana nao. Ahsanteni sana. (*Makof!*)

Tunao pia Viongozi wa Dini kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Sheikh Mustafa Rajab Shaaban ambaye

amekuja kwa niaba ya Sheikh wa Mkoa wa Dodoma; karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Sheikh Kisusu Mrumbo ambaye ni Kadhi wa Mkoa; karibu sana. tunaye pia Alhaj Marusu Matata Msii. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Askofu Dickson Chilongani, Askofu wa Dayosisi ya *Central Tanganyika*. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia *Bishop* Evans Chande ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma; karibu sana. (*Makofi*)

Tunao Wabunge wastaafu waliko hapa na hawa ni marafiki zangu, Mheshimiwa Haroon Pirmohamed. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Haroon Pirmohamed, hayo makofi hayajaja bure na huu ni mwezi Februari tarehe moja, mwezi mzuri kabisa. Kwa hiyo tunaamini utayakumbuka haya makofi ukiondoka halafu utafanya yale mambo yako. Tumeyakumbuka sana nami nltaendelea kukukumbusha ili tusijislikie upweke humu ndani. Maadam leo umetutembelea, tunaomba ukumbuke ule utamaduni wako. Ahsante sana. (*Makofi*)

Yupo pia Mheshimiwa Ester Michael Mmasi; karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hapa nina marafiki wengi lakini nitawaita wote kama kundi na wote watasimama kwa pamoja; marafiki zangu wote wasimame na wao wapunge mikono. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Hawa marafiki wanatoka sehemu mbalimbali lakini kwa sababu ya muda ambao tumeshautumia mpaka sasa na kuna vikao vinafuata baada ya hapa, nisichukue muda wenu mwingi lakini nawashukuru sana maana hawa

wametoka sehemu mbalimbali wamesafiri kuja kushuhudia tukio hili. Ahsanteni sana kwa kuja, Mungu awabariki.

Tunao pia Watumishi wa Umma wa Wilaya na Mkoa wa Mbeya, nao wako hapa. Mungu awabariki sana kwa kuja.

Tunao vijana vile vile ambao huwa wanafanya zile kazi ambazo siku moja hapa Waziri Mkuu alizitambua wakafurahi sana na wao wasimame kwa umoja wao; vijana wa *Tulia Trust*; karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Tunao waandishi wa habari kutoka Mkoa wa Mbeya; karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia viongozi wa bodaboda kutoka Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Ndugu Aliko Fwanda; sijui wamekaa upande gani, karibuni sana, sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Emmanuel Shangai ambao ni familia yake kutoka Ngorongoro Jijini Arusha, ikiongozwa na mke wake, Ndugu Naraha Ndekeyo na wapiga kura wake wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya, Ndugu Ndirango Senge. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wageni wa wagombea wenzangu wa Uspika; wageni watano wa Ndugu Maimuna Kassim ambaye ni mgombea Uspika kutoka Chama cha ADC wakiongozwa na Katibu Mkuu Taifa, Ndugu Doyo Hassan Doyo; wako pale juu, karibuni sana. Nadhani hili nalo litaongezwa kwenye taarifa za huyu dada yangu. Wakati napitia taarifa yake alisema alikuwa mgombea kwenye jimbo la Mheshimiwa Kigua, kwa hiyo bila shaka na hili litaongezeka kwamba aligombea Uspika pia. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi; Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge hapa tutakutana *Speaker's Lounge* kwa ajili ya kikao kwa ajili ya kujadili mambo yatakayokuja mbele yetu kwenye

Bunge hili. Wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukitoka tu hapa naomba tukutane *Speaker's Lounge*.

Pia Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hatukuweza kufanya kile kikao cha kazi jana tutafanya siku ya leo saa nane kamili. Kwa hiyo tukitoka hapa tuelekee Msekwa kwa ajili ya kikao hicho. Ama saa nane imeshapita? Naona kuna watu wanaangalia saa huku wanaona kama mimi sijaangalia saa vizuri, lakini *Briefing* itakuwa saa nane, sasa hivi tunakwenda kwenye Kamati ya Uongozi. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mnaombwa sana wote kuhudhuria kikao hicho muhimu ambacho tutawenza kufanya hilo zoezi.

Tangazo lingine limetoka kwa Katibu wa Bunge; kutakuwa na zoezi la upigaji picha kwenye lango la kuingia Ukumbini baada ya kuahirishwa Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kubaki Ukumbini kwa dakika chache wakati Spika, mimi, nikitoka na viongozi wengine kutoka humu Ukumbini Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mbaki ili tupige picha ya ukumbusho kwenye lango letu kuu hapo. (*Makofii*)

Sasa hili nadhani tutasaidiwa kusomewa na Katibu tutakapokuwa tumetoka pale nje kwa ajili ya makundi yatakayokuwa yanapiga picha. Nimeshauriwa hapa niwatangazie ili tujue utaratibu utakuwaje, kutakuwa na picha ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Spika wa Baraza la Wawakilishi; kutakuwa na picha ya Spika na Maspika Wastaafu; kutakuwa na picha ya Waziri Mkuu, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Maspika wawili Wastaafu, Waziri Mkuu Mstaafu, *Chief Secretary* wa Wakuu wa Mikoa na Katibu wa Bunge.

Halafu kutakuwa na picha ya Meza Kuu na Wakuu wa Vyombo vyta Ulinzi na Usalama; kutakuwa na picha ya wajumbe na Viongozi wa Dini Kitaifa na wale wa Mkoa wa Dodoma na wale wa Mkoa wa Mbeya itakuwa ni picha moja.

Halafu kutakuwa na picha ya hao viongozi pamoja na Machifu; Spika na familia; Spika na wagombea wote wa

Uspika, hii picha itakuwa ya kihistoria. Halafu na picha na Ma-DC na Wenyeviti wa Halmashauri, Viongozi wa CCM na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mameya, Wenyeviti wa Halmashauri na Madiwani wote. Kwa hiyo hapa tutaongozwa na meza ya Katibu, watakuwa wakitusaidia kusoma ili tutoke kwa utaratibu huo.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana na baada ya matangazo haya, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.35 Mchana Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 2 Februari, 2022, Saa Tatu Asubuhij)*